

AINA TATU ZA WAAMINI

 Na tuinamishe vichwa vyetu. Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, pamoja na mioyo yetu, sijui ni wangapi wangetaka kukumbukwa katika maombi, utainua tu mkono wako, useme, “Bwana, nikumbuke, Ee Bwana.” Kuna haja nyingi sana hapa, vitambaa viko juu ya dawati.

² Baba mpendwa wa Mbinguni, tumekusanyika tena jioni hili chini ya dari hili, mahali ambapo umekutana nasi mara nyingi sana, nawe umeonyesha upendo Wako kwetu; tunapojaribu katika njia zetu nyenyekevu kuonyesha upendo wetu na shukrani Kwako, kwa uliyotutendea. Basi usiku wa leo tunakuja tena, Bwana, kama watu wahitaji, kwa maana sisi daima tunakuhitaji Wewe. Na mradi tuko hapa duniani, tunajua hicho ndicho kitakachokuwa kilio, kwa kuwa tuko vitani. Nasi tuna... Vita vinawaka moto, Nawe uliahidi na kusema vile adui angekuwa kama simba angurumaye. Yeye ameachiliwa katikati ya watu, nasi tunaweza kuona jambo hilo kila mahali, kama simba angurumaye akimeza kila awezaye, kwa maana yeye anajua wakati wake ni mfupi. Lakini sisi tuna—tuna Ba—Baba anayewashughulikia watoto Wake, nasi tunakimbilia Kwako na haja zetu, usiku wa leo, Bwana. Tunaomba ya kwamba Wewe utazitimiza.

³ Na vitambaa hivi vilivyowekwa hapa, Baba, vinamaanisha kwamba kuna watu wagonjwa mahali fulani nchini, na ambao wanakuita na kukuhitaji Wewe, na kukuamini Wewe, kuitekeleza imani yao hapa kuleta vitambaa hivi. Mungu, jalia kwamba kila mmoja wao aponywe.

⁴ Tunaona uweza Wako mkuu, Bwana, muda mfupi tu uliopita kule kwenye chumba kile, ukimrudishia kumbukumbu kamilifu mvulana aliyekuwa amepotea. Tunaona uweza Wako ulio mkuu, siku baada ya siku, ukiondoa magonjwa na kufunua siri za moyo, na kuwaonyesha watu, na kuwaweka katika utaratibu moja kwa moja. Tunakushukuru, Bwana Mungu, maana jambo hilo linazidi mwanadamu ye yote. Hilo ni zaidi ya cho chote ambacho ye yote wetu angejua, jinsi Wewe unavyoweza kufichua sababu yake hasa, na nini kimetenda jambo hilo, na jinsi lilivyo. Huyu ni Wewe, Baba. Nasi tunajua, ya kwamba, “Neno Huchunguza moyo, na kama linalotambua mawazo na makusudi ya moyo,” kwa hiyo tunakushukuru kwa ajili ya jambo hili.

⁵ Na sasa, Bwana, tunaamini ya kwamba hao watu sasa, huku vichwa vyao vimeinamishwa, wanatafakari juu ya mambo haya, na ni Roho Mtakatifu anayezungumza nao. Basi jalia kwamba kila moja ya haja zao itimizwe. Waokoe wanaoweza

kuokolewa, Bwana, usiku wa leo. Waliopotea, naomba waingie wakaokolewe.

⁶ Tunashukuru sana kuona lundo lile kubwa mno la nguo zilizolowa maji pale, tukijua ya kwamba kaburi tayari limefunguliwa; na dhambi ya yule mtu wa kale imezikwa, kwa ajili ya wengi wao. Nami nakushukuru kwa jambo hilo, Baba. Basi naomba wao watembe katika upya wa Uzima, siku zao zilizosalia. Katika Jina la Yesu Kristo, tunaomba. Amina.

⁷ Bwana awabariki, ajalie haja uliyokuwa nayo moyoni mwako kujibiwa.

⁸ Naam, ninaamini Billy alisema ya kwamba Ndugu Wheeler alikuwa na mtoto mchanga. Hilo lilikuwa kweli? Nilikosea hapo, kuwekwa wakfu, ama cho chote kile, ama kuweka wakfu. [Ndugu Neville alisema, “Ninaamini kulikuweko na watoto wachanga watatu ama wanne.”—Mh.] Vema. Kama mngetaka kuwaleta sasa, tutafurahi; kama wazee watakuja huku mbele, wawakeke mikono hao jamaa wadogo, kwa ibada ya kuweka wakfu. Nasi tutajaribu kufupisha tu. Na tunataka jamaa hawa wadogo, wanaotaka kuja kwa Bwana Yesu, wanaotaka kuleta vito vya—vyao vidogo walivyopewa na Mungu. Daima sisi hujaribu kuwapa nafasi, kwa maana hatujui ya kesho.

⁹ Mama yangu alizoea kuniambia, “Usiahirishe, kesho, jambo linaloweza kufanywa leo.” Hilo ni kweli, sababu hujui ya kesho, bali tunamjua Yeye anayeshikilia kesho. Hiyo ndiyo sehemu iliyo muhimu. Tunamjua Yeye anayeshikilia kesho.

¹⁰ Ndugu Wheeler, Bwana Mungu akubariki. Na huyu ni Dada Wheeler. Kweli ninafurahi kukutana nawe. Na mimi... majaliwa yangu mema, mara ya kwanza, ninaamini, ni juavyo mimi, kukutana nawe. Na huyu ndiye mtoto wenu mchanga. Jina lake ni nani? [Dada Wheeler anasema, “Carlena Rebecca.”—Mh.] Carlena Rebecca. Naam, kalivyo kasichana kazuri, kazuri kama kawezavyo kuwa. Naam, mtoto Carlena Rebecca Wheeler.

¹¹ Ndugu Wheeler ni mmoja wa mashemasi wetu hapa kanisani, na Mungu ameibariki ndoa yao, kwa mtoto huyu mchanga. Ninaamini mna, yapata, najua, wasichana wengine wawili, sivyo? [Ndugu Wheeler anasema, “Watatu.”—Mh.] Wasichana wengine watatu. Kweli wao ni bibi wazuri, kama ninavyofahamu, na kwa hiyo naomba ya kwamba Mungu atamfanya Rebecca kama hao wengine tu. Mnaona? Na basi jambo hilo litaridhisha kwenu nyote, sivyo? Hilo ni sawa, maana wao ni watoto wanaopendeza sana.

¹² Sijui kama ataniruhusu kumshika ama la, lakini, kama hataniruhusu, tutaweka mikono juu yake. Ungetaka kuja hapa kwangu, Rebecca? Unataka nikushike? Vizuri sana. Jinsi kalivyo kasichana kazuri!

Sasa na tuinamishe vichwa vyetu.

¹³ Baba wa Mbinguni mwenye rehema, tunaposimama hapa mbele ya shemasi huyu, usiku huu; na kwa kweli yeye ameshika kazi nzuri, kwa maana shemasi hana budi awe asiye na hatia, mume wa mke mmoja, akiisimamia jamaa yake vizuri. Kwa kuwa, kama hajui jinsi ya kuisimamia jamaa yake, ataisimamiaje nyumba ya Mungu? Nasi tunakushukuru kwa sababu ndugu huyu ametimiza masharti haya, na ndani yake tunaona Roho wa Mungu.

¹⁴ Naye anamleta sasa binti yake mchanga hapa, awekwe wakfu. Umemweka mikononi mwao wapate kumlea. Mungu, na jinsi tulivyo na shukrani, kwamba tunaweza kusema, mapenzi yao ni kwamba yeye atakuwa kama dada zake wengine. Jalia, Baba, kwamba jambo hili liwe hivyo. Na mtoto huyu na aishi na—na akutumikie sana Wewe, Baba. Na sasa, katika Jina la Yesu Kristo, tunamtoa mtoto huyu Kwako kwa ajili ya maisha ya utumishi. Mpe afya, nguvu; naomba kwamba aishi maisha marefu, hata Yesu atakapokuja, kama hilo linawezekana. Na tena, Baba, tunaamini kwamba yeye atalelewa katika maonyo ya Kristo. Nasi tunayatoa maisha yake Kwako, kwa maisha ya utumishi. Amina.

¹⁵ Mungu akubariki, Rebecca. Na Mungu akubariki, Ndugu Wheeler na Dada Wheeler. Bwana awe pamoja nanyi.

¹⁶ U hali gani? Sasa hapa kuna msichana mwingine mdogo mwenye tabasamu kubwa usoni mwake. Na jina lake ni nani? [Mamaye anasema, “Rhonda Renee Coats.”—Mh.] Rhonda Renee Coats siyo? Mna ukoo na Wakina Jesse na hao wengine, Jesse Coats? [“La.”] Nilifikiria tu...Niliwajua baadhi ya wakina Coats hapa mjini. Niliwajua vizuri sana, nao wamekuwa—wamekuwa rafiki zangu kwa—kwa muda mrefu.

¹⁷ Rhonda, Rhonda Renee. Sijui kama ungekuja kwangu, Rhonda? Nita—nitakurudisha moja kwa moja kwa mama yako, mara baada ya kukutoa kwa Bwana Yesu. Naam, jinsi anavyopendeza!

Sasa na tuinamisha vichwa vyetu.

¹⁸ Baba wa Mbinguni, wakati mimi na mzee Wako tunaposimama pamoja usiku wa leo, katika mapatano na moyo mmoja katika Injili, mama huyu anamleta mtoto huyu Rhonda Renee Kwako kuwekwa wakfu. Umemweka mikononi mwake, amlee, na jambo la kwanza analoweza kufanya ni kumkabidhi Kwako. Kama Ayubu wa zamani za kale alivyosema, Bwana hutoa vitu hivi. Nasi tunaomba, Mungu, ya kwamba utamweka kwa salama mpaka ile saa utakapomchukua. Pia, Mungu, jalia kwamba ataishi maisha halisi ya Mkristo na awe mfano kwa wengine, anapokua. Ibariki nyumba yake, na naomba kwamba iwekwe wakfu Kwako, kwa utumishi mkamilifu, pamoja na mioyo ya kweli. Na sasa, Mungu, tunakupa mtoto Rhonda

Reene Coats, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya maisha ya utumishi. Amina.

Anapendeza sana! Mungu akubariki, dada.

¹⁹ U hali gani! [Yule dada anasema, “Robert Paul Shammel.”] Robert Paul Shane? [“Shammel.”—Mh.] Shammel.

²⁰ Vema, vipi kama... Nawe kwa namna fulani bado u mtoto mdogo bado, sidhani ungalifanya fujo sana juu ya jambo hilo. Usinicheke namna hiyo. Angalia hapa, kama ukitaka kitu cha kucheka. Robert Paul, ni jina zuri namna gani!

Na tuinamishe vichwa vyetu.

²¹ Mungu, wakati msichana huyu mdogo anapokuja hapa; ndiyo hasa, kwetu, angekuwa ni mtoto tu. Naye anamtoa mvulana wake mdogo, Ee Mungu, kama maisha ya utumishi Kwako. Ni tunda na matokeo ya ndoa yao. Ninaomba, Mungu, wakati mimi pamoja na mzee Wako tunapoweka mikono juu ya mshiriki huyu mdogo, ya kwamba maisha yake yatatolewa Kwako. Jalia, Bwana, kama kuna kesho, na auchukue Ujumbe ambao wazazi wa—wake wanausikiliza, Mungu. Jalia jambo hilo. Nami ninaomba ya kwamba Wewe utabariki nyumba zao, na huyu mtoto na alelewe katika maonyo ya Mungu, naye atakuwa m—mfuasi Wako mwenye upendo. Tunamtoa Kwako katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

²² Vema, ye—yeye ni mvulana mmoja tu mzuri. Hivyo tu. Naam, bwana. Usingeomba kitu kingine kipendezacho zaidi, sivyo? Hakuna kitu kingine ulimwenguni kingaliweza kuwa cha kupendeza zaidi, hiyo ni kweli, kuliko jamaa huyo mdogo. Tabasamu tupu! Hilo linapendeza? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

²³ Huo ndio wakati mmoja mke wangu anaonea wivu kazi yangu, kuwashika hao watoto. Yeye anapenda kuwashika. Nami napenda jambo hilo, pia, lakini daima ninahofu nitawavunja. Wao ni nini—hii sana, unajua, ni wazuri sana na wanaonekana wororo sana, lakini, unajua, wao ni—wao ni wagumu kweli kuliko vile ambavyo tungekuwa sisi.

²⁴ Naam, niliwaambia nitatoka... Vema, nina dakika thelathini na tano tu. Itanibidi kuharakisha, sivyo? Hebu tuone. Si—si—simaanishi ku—kutoa uamuzi mbaya kwa jambo lo lote, wala kusema jambo lo lote lisilo sahihi, bali nitajaribu sana, kwa sababu... Unajua, baada ya sisi kuendelea sana katika sa—safari, sisi si—sisi si wenye juhudi kama tulivyozea kuwa, unajua. Zile maili wakati mwingine zinakuwa ngumu, na ibada mbili ama tatu kwa siku, ati... .

²⁵ Na kile kinachosababisha hiyo sehemu muhimu, ni hayo maono. Kuhubiri hakunidhuru. Jamani, ninaweza kusimama hapa siku nzima, wala hilo halitanidhuru, lakini mimi... . Bali tu hayo maono, na wakati watu wako kwenye mazungumzo haya

ya faragha, hayo ndiyo wanayopaswa wao kuyapata. Mnaona? Hilo ndilo lililowaleta hapa. Ni jambo lisiloweza kutatuliwa tu kwa kuwekea mikono. Hapana budi kujua chanzo chake, mwanzo wake, nini kinacholianzisha, nini kilicholisababisha, na halafu jambo la kutenda ili kutoka kwenye jambo hilo. Hilo ndilo lililowaleta hapa.

²⁶ Naam, mkutano unaanza, kesho kutwa usiku... ama, la, samahani, ni Jumatano usiku, huko Shreveport, Louisiana. Na iwapo mmoja wenu ana marafiki karibu na mahali pale, naam, waambieni waje. Maskani ya Uzima, nafikiri, ndipo i— inapoanza, isipokuwa wapate jumba la mikutano, kama wao wanaweza kulipata hilo, ambalo linawapa nafasi zaidi ya kuketi. Bali wao wana roshani huko juu orofani, na ukumbi ule mkuu, halafu chumba kingine chini yake. Kwa hiyo, sijui hasa ni wangapi wanaweza kuketi humo, lakini ni... Mambo yakiwa mabaya sana, labda tunaweza kupata lile jumba la mikutano upande wa pili wake kutoka hapo, ambalo lita... Wala, sijui linaweza kukaa wangapi. Nimekuwa na mikutano kule, bali sikumbuki. Huu ni—ni mkutano wa kila mwaka.

²⁷ Miaka mitatu iliyopita nilikuwa kule chini, nasi tukaanza ufufuo, katika Jina la Bwana, nao haujaisha bado, tangu wakati huo. Unaendelea tu moja kwa moja, moja kwa moja tu; kila siku, watu wanaingia, wanaokolewa, wanabatizwa, nao wanaendelea na Bwana namna hiyo, wahudumu na kila kitu wakiingia moja kwa moja. Nasi tuna nini-hii tu... Mradi unaendelea namna hiyo, nami ninakaa hapa, ninataka kuutembelea wakati wote, na kuingiza tu maneno yangu machache na—na kuendelea.

²⁸ Naam, huo utaanza Jumatano, na kuisha Jumapili. Kifungua kinywa cha Wafanyi Biashara Wakristo ni... Si... nasahau jina la hoteli hiyo... Ninaamini ni ile... inaitwa... Wao, watakwambia utakapofika pale. Ni kifungua kinywa cha wafanyi biashara.

²⁹ Tulikuwa na wakati mzuri sana kule, kwenu wafanyi biashara mlio hapa, wakati wa mwisho kule. Bwana alimwokoara—rabi fulani, kwenye mji huo. Na, loo, sijui yote yale yaliyotukia. Ulikuwa ni wakati mkuu katika Bwana, kule, tukihubiri juu ya lile Agano la Damu. Kwa hiyo sisi... Hilo ndilo Wayahudi wanalojua habari zake; ni ile damu. "Pasipo kumwagika kwa damu, hakuna msamaha," mnaona.

³⁰ Sasa hebu twende moja kwa moja kwenye Neno, nami nitafanya niwezavyo kutunza neno langu.

³¹ Basi sasa, kama Bwana akipenda sasa, Jumapili baada ya Krismasi, kama mko kwenye likizo zenu na mnazunguka kila mahali kwa magari, hakutelezi na kadhalika, mbona, m— mkiwa karibu na hapa, naam, karibuni. Nasi tunakusudia kufanya ibada hapa Jumapili asubuhi, ya—ya—ya Jumapili baada ya Krismasi. Ni tarehe gani wakati huo? [Mtu fulani anasema,

“Ishirini na tisa.”—Mh.] Ishirini na tisa, siku ya ishirini na tisa, na hiyo ni Jumapili baada ya Krismasi, siku ya ishirini na tisa. Naam, kama jambo lo lote likitukia kwamba sisi, kitu fulani, hatutakuwa hapa, na hatuwezi kuwa hapa. . . Hatujui ya usoni, mwajua. Lakini kama jambo lo lote likitukia, mbona, ninyi mnaokaa nje ya mji, ambao mmekuja, kama hawa watu kutoka huko Memphis. . .

³² Nilitaka kumsikia Ndugu Ungren akiimba *Jinsi Wewe Ulivyo Mkuu*. Nami si- . . . Yeye yuko hapa usiku huu?

³³ Basi, kwa hiyo, nami daima nina mambo mengi sana, siwezi kumaliza kuyafanya yote, siwezi kumaliza kuyafanya yote. Mungu awabariki, enyi watu.

³⁴ Sasa hebu tufungue kwenye Maandiko sasa kwa ajili ya kusoma Maandiko ki—kidogo. Ambapo, kama maneno yangu yakishindwa, Hili halitashindwa. Na basi Mungu atawabariki kwa kukaa, kwa ajili tu ya kulisikiliza Neno Lake. “Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno la Mungu.” Hiyo ni kweli? Sasa nilivyokuwa nikifikiri. . . Wakati, mnapofungua Yohana Mtakatifu sura ya 6, kuanzia aya ya 60, na kusoma ya 71, zote pamoja. Yohana Mtakatifu 6:60.

³⁵ Sasa nilikuwa nikifikiria, huku nikiangalia nje ya dirisha muda kidogo uliopita, huku nikiangalia kutua kwa jua na kuona jinsi maumbile yote yalivyo na sheria. Na majira ya kipupwe yanapokuja, ile sheria, yenyewe tu, ya maumbile, inaupeleka utomvu chini kwenye mizizi ya mti. Unazikwa.

³⁶ Kama alivyosema Ayubu, “Loo, laiti ungenificha kuzimuni, ukanilinda kwa siri hata gadhabu Zako zitakapopita.” Na sasa, ni hivyo, “Laiti ungenificha!” Mnaona, yeye aliona ma—maumbile, mti, uhai ukishuka kwenda kwenye mizizi; Ndugu Way. “Ndipo nikae huko hata gadhabu zako zitakapopita, kisha uniite na kuniambia wakati.” Mnaona?

³⁷ Maumbile yana sheria. Kuna sheria ya maumbile; hakuna njia kamwe ya kuepuka jambo hilo. Ni sheria ya maumbile. Halafu tena kuna sheria ya roho; kuna, pia, hakuna njia ya kuepa jambo hilo.

³⁸ Nilikuwa ninazungumza na mtu na mke alasiri ya leo, kuhusu, huwezi kuangamiza kitu cho chote kabisa. Wanadamu hawawezi kuangamiza kabisa. Wanaweza kuvunja, bali si kuangamiza kabisa. Ndipo mtu fulani akasema, “Vema, vipi kuhusu kuchukua na kuchoma kipande cha karatasi, hilo linakiangamiza kabisa?” La, bwana. Hilo linavunja-vunja tu zile kemikali, joto la moto. Kinarudi moja kwa moja kwenye gesi, jinsi ilivyokuwa hapo mwanzo. Huwezi kuangamiza kabisa. Na iwapo ulimwengu ungesimama muda mrefu vya kutosha, gesi zizo hizo, hizo na—na kemikali zilizokuwa kwenye karatasi hiyo, zingeweza kurudi moja kwa moja na kuwa kipande cha karatasi tena. Hiyo ni kweli. Huwezi kuangamiza kabisa. Kweli.

³⁹ Mungu, basi. Kama kuna ufufuo kwa kila kitu, kurudi tena, na hakuna kuangamiza kabisa, kuna ufufuo wa wenye haki, naam, nasi hatuna budi kurudi. Hakuna lingine. Hakuna njia kamwe ya kufanya jambo hilo. Haidhuru kama umeteketewa, kama umekufa kwa maji, po pote jambo hilo linapotukia, wao hawawezi kuangamiza kabisa.

⁴⁰ Kumbuka tu ya kwamba kila sehemu yako ilikuwa hapa, wakati Mungu aliponena ulimwengu ukawa. Yeye aliweka mwili wako wakati uo huo. Wala hakuna kitu kinachoweza kuuondoa ila Mungu. Yote yamerudi mikononi Mwake tena. Mnaona? Naye Ndiye—Ndiye, Mu—Muumba, Ndiye aliyetoa ahadi, kwa hiyo tuna hakika kwamba kuna Uzima wa Milele. Nasi tuna uhakika moyoni mwetu sasa, ya kwamba sasa tuna Uzima wa Milele, Uzima wa Milele ambao hauwezi kufa, ndani mwetu sasa. Vema.

⁴¹ Yohana Mtakatifu 6. Hebu na tuanze sasa na sura ya 6 ya Yohana Mtakatifu, na kuanzia aya ya 60.

Basi watu wengi miongoni mwa wanafunzi wake waliposikia, waliposikia, walisema, Neno hili ni gumu, ni nani awezaye kulisikia?

Basi Yesu akafahamu nafsini mwake ya kuwa wanafunzi wake wanalinung'unikia neno hilo, akawaambia, Je! neno hili linawakwaza ninyi?

Itakuwaje . . . mmwonapo Mwana wa Adamu anapaa huko alikokuwako kwanza?

Ni—ni . . . roho ndiyo itiayo uzima, nao mwili haufai kitu; maneno hayo niliyowaambia ni roho (huyo ni Yeye), tena ni uzima. (Yeye alisema nini? “Mimi ndimi Kweli, Uzima.”) . . . ni roho . . . ni uzima.

Lakini kuna wengine miongoni mwenu wasioamini. Kwa maana Yesu alijua tangu mwanzo ni nani wasioamini, naye ni nani atakayemsaliti.

Akasema, Kwa sababu hiyo niliwaambia ya kwamba hakuna mtu awezaye kuja kwangu isipokuwa amejaliwa na Baba yangu.

Basi kwa ajili ya hayo wengi miongoni mwa wanafunzi wake wakarejea nyuma, wasiandamane naye tena. (“Maneno magumu,” mnaona, yeye asingestahimili jambo hilo.)

Basi Yesu akawaambia wale thenashara, Je! ninyi nanyi mwataka kuondoka?

Basi Simoni Petro akamjibu, Bwana! twende kwa nani? Kwa kuwa wewe unayo maneno ya uzima wa milele.

Nasi tumesadiki hivyo, tena tumejua ya kuwa wewe ndiwe Kristo, Mtakatifu wa Mungu. (Jamani!)

Yesu akamjibu, Je mimi sikuwachagua ninyi thenashara, na mmoja wenu ni shetani?

Alimnena Yuda, mwana wa Simoni Iskariote; maana huyo ndiye atakayemsaliti; naye ni mmojawapo wa wale thenashara.

⁴² Naam, kama ningeliliita hili somo kwa ajili ya usiku huu, na kujaribu niwezavyo kufanya hiyo nusu saa iwe na maana, nataka kuzungumzia juu ya: *Aina Tatu za Waamini*.

⁴³ Nami mara nyingi nimetoa tamshi. Nami niliwaza, “Vema, nitaamini tu nitahubiri juu yake wakati mmoja, alasiri ya leo.” Niliwaza hilo.

⁴⁴ Wa, kwanza, ni waamini, waamini wa kujifanya, na wasioamini. Naam, hilo kweli ni...nanyi...somo. Lakini, kwa hakika kama tunavyoketi hapa usiku huu, kundi hilo daima linakusanyika pamoja. Po pote wanapokusanyika watu, tunakuta kundi hili, na daima tumewapata, na labda daima tutakuwa nao hata Kuja kwa Bwana. Nami nataka sisi, usiku huu, kujiangalia wenyewe, ninapozungumza juu ya makundi haya matatu, tuone tumo kwenye kundi lipi.

⁴⁵ Sasa kumbukeni, ninazungumza hapa labda...Kanisa hili, lililojaa tena usiku huu, kila mahali, na kuta na vinjia, lakini pia ninazungumza na ulimwengu mzima. Mnaona? Kwenye sehemu mbalimbali ulimwenguni, kanda hizi zinakopita, huduma za kanda.

⁴⁶ Sasa nataka kuzungumza juu ya hizi aina tatu za waamini sasa. Sasa kumbukeni, *waamini*, somo langu ni *waamini*. Mmoja wao ni mwamini wa kweli, na mwingine ni mwamini wa kujifanya, na anayefuata ni asiyeamini. Mnaona?

⁴⁷ Naam, kundi la kwanza tungetaka kuzungumzia habari zake, ni mwamini. Kwa sababu, nafikiri anapaswa kuwa wa kwanza, kwa sababu ndiye kweli anayeamini, sasa, anaamini kama wanafunzi walivyoamini hapa. Tutatumia Maandiko haya yaliyosomwa kama mfano. Naam, wa kwanza ni waamini, waamini halisi. “Nayo imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno la Mungu,” Neno la Mungu, ambalo ni Kristo. Mnaona, waamini!

⁴⁸ Naam, mliliona tamshi hili muhimu sana ambalo mwamini huyu alitoa? Naam, mwamini si lazima awe ni mtu mwerevu katika namna ya ulimwengu ya kuwa mwerevu. Si lazima awe ni mtu mwenye elimu kwa jinsi ambavyo watu hawa wanajaribu ku—kusema kwamba huna budi kuwa; bali si lazima. Wewe... Mtu huyu aliyetoa tamshi hili, Biblia yenyewe ilisema yeye alikuwa “asiye na elimu” wala “maarifa”. Petro, yeye kweli hakuonekana kwamba ni mtu mwenye akili.

⁴⁹ Katika Isaya 35, inasema, “Kutakuwako na njia kuu, na njia, nayo itaitwa, ‘Njia ya utakatifu.’ Wasio safi hawatapita juu yake.”

⁵⁰ Nilikuwa nikizungumza na mmoja wa mashemasi alasiri ya leo, tulipokuwa tukizungumza juu ya madaraja yanayounganisha upande mmoja na mwingine, na hili jipya. Nikasema, “Kuna madaraja mengi kuvuka maji mengi, ya ghuba leo.” Kisha nikasema, “Lakini kuna daraja moja kuu leo ambalo limetokea duniani kufikia hadi Utukufuni, huitwa, ‘Njia Kuu ya Mfalme.’ Wasio safi hawatapita juu yake.” Hiyo ni kweli. Ni njia—njia iliyojengwa na Kristo Bwana wetu, daraja lililofanywa kutoka dunia hii mpaka kwenye Nchi nyingine, wasio safi hawaipitii.

⁵¹ Petro, mtu huyu asiye na maarifa, wa . . . akisimama karibu, alipokwisha kuona Neno la siku hiyo lililo—lililothibitishwa kwelikweli, ambalo Mungu aliahidi katika siku hiyo ya kwamba kungekuweko na Mmoja atakayeinuka ambaye angekuwa Na—Nabii kati yao. Na ilikuwa vigumu kwa Simoni kuliadini, kwa kuwa kungekuweko na miigizo mingi ya Jambo Hilo. Bali alipoona Neno halisi na lililofunuliwa la wakati huo, na kumsikia Yeye akijitambulisha barabara, yeye—yeye alisadikishwa hakika Yeye kwamba alikuwa ni Nani. Naye alikuwa ndiye, aliyesema, “Bwana, twende kwa nani?” alipoulizwa.

⁵² Wakati u—umati ulipokuwa ukitengana, kati ya waamini, na wasioamini, na waamini wa kujifanya, walikuwepo wote watatu wakiwa wamesimmama pale pale katika kundi hilo moja la watu; waamini, waamini wa kujifanya, na wasioamini, wanaopatikana papa hapa katika sura hii. Na kwa kuwa Yesu alikuwa amenena hayo Maneno jinsi alivyoyanena, hilo lilitenganisha kusanyiko Lake. Lakini halina budi kutendwa.

⁵³ Yeye alikuwa mtu mashuhuri mradi tu aliwaponya wagonjwa, bali ilipofikia kwenye Mafundisho na unabii, hilo ndilo lililotenganisha ma—makapi na ngano. Mnaona? Makapi huifunika tu ngano. Siyo ngano. Hayawezi kutumiwa. Hamna cho chote ndani yake. Hamna Uhai ndani yake. Ni ganda, nalo haliwezi kukaa pamoja na ngano. Halitarithi pamoja na ngano. Na kwa hiyo labidi . . . Ngano tu ndiyo tunayonena habari zake, kile kiini cha punje ya ngano.

⁵⁴ Sasa angalieni, Petro alikuwa ameshawishika kwamba huyo alikuwa ndiye Masihi. Naam, haidhuru wengine wote walisema kitu gani. Haidhuru makuhani walisema kitu gani. Haikujalisha kwa Simoni Petro kanisa lilisema nini. Yeye alikuwa ameaminishwa, yeye mwenyewe.

⁵⁵ Yesu alimwambia, katika mahali fulani Yeye alipouliza, “Watu huninena kwamba Mimi ni nani?”

56 “Na wengine walisema Wewe ni ‘nabii,’ na wengine walisema Wewe ni ‘mmoja wa manabii wa kale aliyefufuka,’ na—na Wewe ni ‘Musa,’ ama ‘Eliya,’ ama mtu fulani.”

Yeye akasema, “Nimewauliza *ninyi*. Mnafikiri nini?”

57 Ndipo Petro akasema, “Wewe ni Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai.”

58 Yeye akasema, “Heri wewe, Bar-yona, Simoni, Bar-yona; kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili kamwe. Wewe hukujifunza jambo hilo kwenye kitabu, ama kutoka kwenye kanuni fulani ya imani, ama kutoka kwenye katekismo fulani. Wewe...Baba Yangu, aliye Mbinguni, amekufunulia jambo hili.” Huyu hapo mwamini halisi; ufunuo wa kiroho wa Neno. Mnaona? Na ju-... “Wewe ni Simoni, na juu ya mwamba huu, wa ufunuo wa Mimi ni nani, nitalijenga Kanisa Langu, wala milango ya kuzimu haiwezi kulishinda.” Mnaona?

Si ajabu Simoni alisema, “Twende kwa nani?”

Yesu aligeuka na kusema, “Je! ninyi nanyi mwataka kuondoka pia?”

59 Nao wakasema, “Bwana, sisi twende, twende kwa nani? Kwa kuwa, Wewe pekee ndiwe uliye na Maneno ya Uzima wa Milele. Wewe Ndiwe pekee.”

60 Kwa kuwa, Yeye hakuwa tu na Maneno ya Uzima wa Milele, Yeye alikuwa Neno la Uzima. Mnaona. Yeye alikuwa ndiye lile Neno la Uzima, naye Simoni alitambua jambo hili barabara. Basi alipolitambua, hilo ndilo lililoshikilia nanga yake, kwa maana ilifunuliwa kwake ya kwamba Yeye alikuwa ndiye lile Neno lililo hai.

61 Naam, huyo ndiye mwamini halisi, wakati Roho Mtakatifu; si kushawishiwa fulani na mtu fulani mwingine, si kwa kitu kingine fulani. Bali wakati Roho Mtakatifu amekufunulia Neno Lenyewe, nawe unaona Neno limefanywa dhahiri, limethibitishwa; ndipo Roho wa Mungu anakuja na kuingia katika wakati huo, kwa ajili ya Neno la wakati huo, na kulidhihirisha.

62 Mtu angalijizuiaje kumwamini Luther kama alijua jambo hilo? Luther alikuwa mtengenezaji. Roho wa mtu alitoka akaenda pale kwa ajili ya matengenezo. Wesley, vile vile. Ilibidi waliamini. Mnaona, huo ulikuwa ule—huo ulikuwa ni ujumbe kwa wakati wa kanisa. Hilo ndilo lililotukia hasa. Hilo ndilo ambalo lilipaswa kutendeka. Ilikubidi uliamini.

63 Nasi hapa tumefikia, tumefikia Wakati wa Laodikia. Nasi tumefundishwa, katika Wakati wa Laodikia, ya kwamba Kristo aliwekwa nje ya kanisa Lake; Naye hata alikuwa anabisha mlango, akijaribu kurudi ndani. Kwa hiyo tunapoona jambo hilo likitendeka, tunajua ni wakati gani tunaishi.

⁶⁴ Halafu, basi, tuko kwenye mwisho wa historia ya ulimwengu. Kitabu sasa kinamaliziwa. Mstari wa mwisho utachorwa kutoka upande mmoja wake hata mwingine siku moja, [Ndugu Branham anapiga makofi mara moja—Mh.] nacho kitafungwa, halafu hapatakuwako na wakati zaidi.

⁶⁵ Basi kuna mchezo mashuhuri wa kuigiza unaotayarishwa. Nao Malaika wamesimama mbinguni, wakiangalia. Mnajua mchezo wa kuigiza ni kitu gani. Wachezaji wako tayari. Mnaweza kuwaona wakicheza.

⁶⁶ Mnaweza kumwona yule mwovu akicheza. Mnaweza kumwona yule mlaghai wa huo mchezo, jinsi alivyoingia jukwaani na ujanja wake, apate kudanganya.

⁶⁷ Lakini pia unaweza kuliona Kanisa lililonyakuliwa likijitayarisha. Ni onyesho kuu sana. Unaweza kuona Uwepo wa Mungu ukithibitisha na kuufanya huo mchezo mashuhuri uliotabiriwa hapa kwenye Biblia hii, kutendeka. Ni wakati mzuri jinsi gani wa kuishi, wakati mtukufu mno kuliko nyakati zote! Watu wa nyakati zote wamekuwa na shauku sana ya wakati huu. Manabii wa kale walitamani sana kuuona wakati huu, bali hawakujaliwa.

⁶⁸ Naam, kulikuweko na mwamini. Kwa sababu, yeye aliliona. Aliliamini. “Sisi tumeshawishika kabisa kwamba Wewe ni Kristo, Yule Masihi, Neno la Mungu kwa ajili ya siku hii, nasi tunaamini jambo hilo.” Mnaona, huyo alikuwa mwamini halisi.

⁶⁹ Hebu tu na tuchukue waamini wengine wachache, upesi sana, kabla hatujaendea aina inayofuata. Hebu tumchukue yule nabii, Nuhu. Wakati yeye, akiwa labda mkulima, labda alikuwa katika zamani hizo, ni mkulima. Bali wakati wenye kudhihaki pamoja na wanadini wa zamani hizo... Kanisa lilikuwa kwenye kiwango cha chini, ndipo Mungu akanena na Nuhu, akamwambia Nuhu ya kwamba yeye ilimbidi ajenge safina. Nuhu hakuhojiana na Mungu jambo hilo. Aliliamini, kwamba lilikuwa ni Neno la Mungu, kisha akatoka akaenda kufanya kazi mara moja akitayarisha mambo.

⁷⁰ Huyo ni mwamini halisi. Usizozane kuhusu jambo hilo. Wakati umeshawishika kwelikweli, basi. Ni kama mtu ye yote, imani yo yote, njia yo yote. “Imani chanzo chake ni kusikia.” Kama unaweza kusimama hapa, haidhuru daktari anasema una shida gani! Ambalo, mtu huyo amekupima magonjwa, na labda anajua tu anachosema, kulingana na yale chombo chake na maarifa yake yatamruhusu kujua, lakini anasema hakuna kilichosalia ila mauti. Lakini, wewe unaomba, na ukisimama kule katika siku za usoni unaweza kumwona mwanamume ama mwanamke mwenye afya amesimama pale. Naam, ni hilo tu. Na jambo ndilo hilo tu. Wao wataendea jambo hilo moja kwa moja na kuingia katika jambo hilo bila shaka, kwa maana wewe unaliamini. Mungu amelinena. Unajua ndivyo ilivyo.

⁷¹ Kama maskini mwanamke yule anayekohoa ile kansa, unaona. Hapakuwepo na tashwishi moyoni mwake. Hilo lingetukia. Ile kansa ilikuwa imekufa, nayo ikajing'oa ikatoka. Mnaona? Naam basi. Unaliamini.

⁷² Kama yule baba aliyemleta mvulana wake mdogo, muda mfupi uliopita, mle ndani. Naye yuko hapa mahali fulani humu jengoni sasa. Maskini mvulana huyo alianguka, akapoteza fahamu zake. Hakuweza kukumbuka jambo lo lote. Punde tu, baada ya maombi, nilimuuliza jina lake. Naye akaniambia umri wake, naye huyo hapo akiwa mzima kama mvulana ye yote angeweza kuwa. Unaona? Wanaamini. Basi Mungu anaposema jambo lo lote, halina budi kuwa namna hiyo.

Basi Nuhu alimwamini Mungu, na Nuhu alihesabiwa kuwa ni mwamini.

⁷³ Danieli, wakati kanisa lilipokuwa utumwani huko Babeli, Danieli alimwamini Mungu. Na haidhuru walisema mambo mengi kiasi gani, “Tutatoa tangazo. Wao hawatamwomba dua mungu mwingine ila sanamu hii iliyo huku nje,” ya mtu huyu mtakatifu, ama cho chote kile. Danieli hakujali cho chote cha jambo hilo. Yeye alikuwa amemsikia Mungu, kwa kuwa alikuwa nabii, nalo Neno lilimjia. Na wakati hekalu lilipowekwa wakfu, ilisemwa, “Kama mtu ye yote ana shida katika nchi yo yote, naye aangalie upande huu kuelekea mahali hapa patakatifu, na kuomba, basi sikia kutoka Mbinguni.” Naye Danieli alimwamini Mungu. Alikuwa mwamini wa kweli, na hata simba hawakuweza kumla. Na hiyo ni kweli, mnaona, yeye alikuwa mwamini. Alikuwa na kitu fulani halisi na cha kweli. Alikuwa ni mwamini.

Daudi, mwamini mwingine, mvulana maskini mdogo.

⁷⁴ Danieli hakushirikiana na kanisa la kisasa, wala Nuhu hakushirikiana na kanisa la kisasa. Hata kidogo. Wao walikuwa ni waamini kwa yale Mungu aliyosema kuwa ni Kweli. Haidhuru ulimwengu wa kisasa ulisema nini, wao waliamini alilosema Mungu lilikuwa ni Kweli. Hao ndio waamini wa kweli.

⁷⁵ Jinsi tu alivyofanya Petro, na wale mitume, wao waliamini Yeye alikuwa na Neno la Uzima na alikuwa Neno la Uzima. Ninaamini jambo lile lile leo. Na kila kitu kingine dhidi Yake ni kinyume, hakiko, ni mauti. *Hili* peke yake ndilo Neno la Uzima, naye Kristo ndiye Neno.

⁷⁶ Naam, Daudi, jamaa mwekundu. Kwanza, yeye labda alichokozwa na nduguze, maana alikuwa jamaa mdogo. Hakuwa mkubwa vya kutosha kubeba silaha. Asingeweza kwenda vitani, naye alikuwa mdogo mno na amekonda. Na, hata hivyo, alikwenda nje huko, kama mwamini.

⁷⁷ Basi alipoketi kule nyuma jangwani, akiangalia kondoo dazani cha—chache ambazo babaye alimpa kuzichunga, akiwa na kombeo, katika nchi ambamo kuna simba na dubu na mbwa mwitu, na kadhalika. Daudi alianza kuangalia kwenye malisho

ya kijani kibichi yenye uvuli, naye alijua ilichomaanisha kwa kondoo kukaa kwenye kile kivuli, na kulala katika joto la jua; alijua umuhimu wa maji mazuri baridi, kama alivyosema, “Kama vile ayala aioneavyo shauku mito ya maji, nafsi yangu inakuonea kiu, Ee Mungu.” Unaona? Yeye alikuwa amelia, ameomba.

⁷⁸ Basi wakati mmoja jambo la dharura likatukia, simba akamshika mmoja wa kondoo zake, akakimbia. Yeye akawaza, “Mungu aliyenifanya nisishindwe na yule simba!” Unaona? Basi akachukua kombeo akamwangusha chini yule simba, akiwa na jiwe dogo kwenye kombeo. Naam, kama mtu ye yote alipata kumwona simba, mmoja wa hao simba wa Afrika, simba wakubwa wenye sufu shingoni walio nao kule Palestina na Asia, wangejua vile mmoja wa hao jamaa alivyokuwa. Ambapo, bunduki kubwa mno ya magnum mia tatu ni vigumu kumwangusha chini, naye akamwangusha kwa jiwe. Na wakati huyo simba alipoinuka amvamie, alimshika haraka kwenye ndevu akamuua. Hiyo ndiyo sababu alijua alichokuwa ananena; yeye alikuwa ameshakwisha pata tukio. Alikuwa amemjaribu Mungu, kuhusu Neno Lake.

⁷⁹ Naye—naye hakumwogopa Goliathi, kwa sababu, yeye hakuwa ametahiriwa. Yeye hakuwa mwamini, hata kidogo; na Goliathi alipotoka na kumlaani katika jina la miungu wake.

⁸⁰ Naye Goliathi, mkubwa mara nyingi kuliko alivyokuwa; mtu mkubwa mno, mwenye vidole vya inchi kumi na nne. Naam, vidole hivyo vingekuwa virefu namna *hiyo*, unaona, vidole vya inchi kumi na nne, shujaa wa vita. Na labda koti la msumari alilokuwa amevalia, labda lina uzito wa ratili mia tatu, ama zaidi, mnaona, alilokuwa amevaa. Chapeo, na nini hii kuu... labda hicho chuma chenye unene wa inchi moja na nusu. Jitu kubwa namna hiyo, likitembea na—na boriti ya mfumaji ambayo inadaiwa kuwa kama futi ishirini. Alikuwa na mkuki wa futi ishirini mkononi mwake. Basi angewezaje mtu ye yote... Mtu kama huyo angalisimama tu na kuokota watu dazani moja, na kuwatupa namna *hiyo*, wanapomjia. Ni upinzani ulioje!

⁸¹ Naye huyo hapo, amesimama pale, akijigamba, kujivuna. Wakati nini hii... inaonekana kama kwamba hawana nafasi, unaona, akasema, “Hebu... Msimwage damu yo yote.” Kasema, “Hebu—hebu acheni mtu fulani aje anipige mimi, na basi kama nikishinda, basi nyote mnitumikie tu; halafu basi kama—kama—kama mkishinda, basi tutawatumikia.” Mnaona, wakati ibilisi anapofikiri ana uwezo wa kukushinda, mnaona, hapo ndipo anapotaka kujigamba. Bali alikabiliana na mtu tofauti. Alikabiliana na mtu aliye mdogo kuliko wote nchini humo, jamaa mdogo, aliyeinama mabega, mwekundu.

⁸² Akasema, “Hivi mnataka kuniambia ya kwamba ninyi, je—jeshi la Mungu aliye hai, litasimama pale na kumwachilia

huyo Mfilisti asiyetahiriwa alitukane jeshi la Mungu aliye hai?" Mbona, yeye alishtushwa na jambo hilo! Kwa nini? Kwa nini? Alikuwa mwamini. Hao wengine walikuwa waamini wa kujifanya. Unaona? Unaona, yeye alikuwa mwamini halisi. Alisema, "Kama mnaogopa, nitaondoka niende nikampige." Mnaona? Ni sai la namna gani kwa kijitu kidogo kama hicho! Na kwa hiyo yeye alikuwa ni mwamini, naye alitenda sawasawa kabisa na aliyojua kwamba Mungu angefanya. Yeye ni . . .

⁸³ Wakati huyo Mfilisti asiyetahiriwa alipomlaani kwa jina la miungu yake, yeye alisema, "Je! mimi ni mbwa; maskini kitoto kidogo kilichodumaa kinijie namna hiyo? Mbona," akasema, "Nitakuokota kwa ncha ya mkuki wangu, kisha nitakuangika kule mtini na kuwaacha ndege wale nyama yako." Loo, jamani! Loo, jinsi alivyokuwa mtu wa kutisha!

⁸⁴ Daudi alisema, "Wewe unanijia kwa upanga na mkuki, na silaha. Unanijia kwa jina la Mfilisti. Bali, ninakujia bila upanga wala mkuki, silaha, bali ninakujia katika Jina la Bwana Mungu wa Israeli."

⁸⁵ Naam basi. Huyu ndiye mwamini. Hilo ndilo ngome yake. Hilo ndilo ngao yake. Hilo ndilo ulinzi wake. Amina! Hilo linapaswa kuwa ndilo ulinzi wa Kanisa. Mwamini ye yote, Hilo ndilo ulinzi wake. Hata kutokee nini, ulimwengu useme nini, cho chote kile, ulinzi wako ni Bwana Mungu wa Israeli. Hilo tu. "Jina la Yesu Kristo ni ngome imara, wenye haki huikimbilia wakawa salama." Hilo ndilo ulinzi wetu, ni Yesu Kristo.

⁸⁶ Angalia, na lilipotukia, tunajua kilichotukia. Daudi, hakuwa na mahali po pote pa kupiga ila mahali pamoja padogo wakati aliposhusha kifuniko cha—cha—chake kwenye uso wake. Mahali pamoja pa kupiga palikuwa papa hapa kwenye paji la uso wake. Na kabla hajalikaribia lile ji—jitu, Mungu alielekeza kwenye ile sehemu ya kuulia, ndipo akaliua lile jitu. Mnaona? Mungu alifanya jambo hilo. Naam, tunaona yeye alikuwa mwamini.

⁸⁷ Naam, mwamini mwingine alikuwa Ibrahimu, naye alikuwa wa . . . Mkaldayo wa mji wa Uri. Naye aliitwa kufanya jambo lililokuwa . . . na kuamini jambo lililokuwa kabisa haliwezekani kwa kimwili. "Lakini hakisita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini," inasema Warumi 4, "lakini alitiwa nguvu, akimtukuza Mungu."

⁸⁸ Wakati Ibrahimu alipokuwa na umri wa miaka sabini na mitano, na mkewe miaka sitini na mitano, nao wameishi pamoja tangu walipokuwa wavulana wadogo. Ilikuwa ni dada yake wa kukeni; mvulana mdogo na msichana mdogo. Na hiyo ilikuwa, wao walikuwa wameishi pamoja, pasipo na watoto kabisa. Basi Mungu akamwambia Ibrahimu, "Jitenge na wasioamini." Mungu daima huita kutoka, mtengano. "Jitenge na wasioamini ukatembee pamoja Nami, Nami nimekufanya baba wa mataifa wengi. Tayari nimefanya jambo hilo."

⁸⁹ Naye Ibrahimu akaliamini jambo hilo. Huyu ni mwamini. “Utafanya jambo hilo namna gani, Bwana?” yeye hakuuliza swali hilo. Mungu alisema angefanya hivyo, na hilo lilitosha.

⁹⁰ Wakati mwezi wa kwanza ulipopita, naye Sara alikuwa angali... Alikuwa ameacha kupata hedhi. “Kuna tofauti yo yote?”

“Hakuna cho chote.”

⁹¹ Bali Ibrahimu bado aliamini jambo hilo. Miaka ishirini na mitano baadaye, kungali hakukuwa na tofauti yo yote, bali Ibrahimu angali aliamini hilo. Huyu ni mwamini. Huyu si anayejifanya mwamini. Huyu ni mwamini. Miaka ishirini na mitano baadaye, Ibrahimu alikuwa na nguvu zaidi kuliko alivyokuwa wakati wa kwanza. “Alimwamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa ni haki.” Kwa kuwa alimwa-... Huyu ndiye mwamini halisi.

⁹² Naam, baada ya kitambo kidogo nitawaacha mchunguze muone mko katika tabaka gani.

⁹³ Basi Ibrahimu alifanya kitu gani? “Hakusitasita katika ahadi ya Mungu,” yasiyowezekana.

⁹⁴ Mtu mwenye umri wa miaka sabini na mitano, akiwa na mke mwenye umri wa miaka sitini na mitano, angefanyaje, kama wao wangeenda kwa daktari na kusema, “Tunataka kufanya matayarisho, hospitali. Tutapata mtoto”? Na halafu, miaka ishirini na mitano baadaye, waseme, “Dakta, ungali umeweka nafasi hospitalini?” Mnaona? Mnaona?

⁹⁵ Linakufanya utende kiajabu. Maamuzi yako ni ya kipekee pekee, kwa ulimwengu. Lakini ni mwamini, hata lionekane geni namna gani. Biblia ilisema, ya kwamba, “Yeye alishawishika kabisa ya kwamba Mungu alikuwa anaweza kutekeleza yale aliyokuwa amesema angefanya.”

⁹⁶ Hilo linapaswa kutendeka kwa kila mwamini alasiri ya leo. Mungu anaweza kutimiza kila Neno alilosema angetimiza. Sijali madhehebu yanasema nini, na maneno, “Siku ya miujiza imepita, na haya yote ni uwezo wa kuwasiliana kimawazo na kadhalika, ni kuagua. Ni...” Haijalishi kwangu wanayosema. Ningali ninaamini. Kama bunduki hiyo imeelekezwa kwenye shabaha, itapiga kwenye shabaha. Nami ninaamini kwamba kama mwamini ameelekezwa kwenye Neno la Mungu, litapiga kitu kile kile. Kama Neno la Mungu limewahi kuahidi jambo hilo, litafanya hivyo tena. Mimi nimeshawishika kabisa kuhusu jambo hilo. Ya kwamba, tunapooni tuko katika wakati huu wakati linapaswa kuwa hapa, linapaswa kuwa hapa. Mambo haya yanapaswa kutukia.

⁹⁷ Hiyo ndiyo sababu ninaamini ya kwamba wakati Bibi-arusi huyo ameitwa na kuteuliwa, na kuandikwa katika Kitabu cha Uzima, itakuja sauti kutoka Mbinguni ambayo italeti ubatizo

mkubwa sana wa Roho Mtakatifu katika Bibi-arusi huyo ambao utamwondoa duniani, katika neema ya Kunyakuliwa. Mungu aliahidi jambo hilo. Sijali ni sayansi ngapi, na ni wanaanga wangapi waliowatuma kwenda angani, na cho chote kile, na ni maili milioni ngapi wanazoweza kuona; sijali cho chote juu ya jambo hilo. Kuna Mbinguni, na kuna Yesu Kristo wa kweli Kule atakayekuja katika mwili kulipokea Kanisa Lake Kwake. Haidhuru hiyo hadithi inaonekana ya kale namna gani, ingali ni Kweli. Mungu alisema jambo hilo. Hilo—hilo ndilo waamini wanaloamini.

⁹⁸ Mungu alisema, “Mimi ni Bwana nikuponyaye magonjwa yako yote. Mimi ni Mungu wala sibatiliki.” Amina! Naye Mungu ni Neno. Basi iwapo Mungu habadiliki, Neno litabadilikaje? Mnaona? “Mimi ni Mungu, wala sibatiliki.” Maandiko yanasema hivyo. Mungu alisema jambo hilo, Yeye Mwenyewe. Na iwapo hawezi kubadilika, basi Yeye ni Neno. “Hapo mwanzo alikuweko Neno, Naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu.” Neno lisilobadilika! “Naye Neno akafanyika mwili, akakaa kwetu.” Amina! Naam, bwana.

⁹⁹ Mungu aliinua miili, nyakati zote; Musa, na Ezekieli, na Yeremia, na Isaya, na Eliya, wakati wote, ambamo Neno Lake lilikuja kwa muda. Bali Neno kamili lilidhihirishwa katika Mtu huyu Yesu Kristo. Ambaye, alikuwa ni Mungu katika—Mungu katika ukamilifu wa Kiungu katika jinsi ya mwili. Hapo alifanyika mwili. Ninaamini jambo hilo, kila Neno.

Ayubu, mwamini mwingine.

¹⁰⁰ Mara kwa mara, waamini hujaribiwa. Si mara kwa mara; kila wakati! “Kwa maana kila mwana anayekuja kwa Mungu hana budi kurudiwa, kujaribiwa, afunzwe kama mtoto.” Kumbukeni, hayo majaribu, zile barabara zenye mavumbi, joto la jua la mateso, lakini uaminifu wa moyo wako unavifua vitu hivyo mpaka vinakuwa tayari kufinyangwa. Watoto wa Mungu wametengenezwa barabara kwa Neno Lake, kwa kuwa wao ni mifano iliyo hai, nalo Neno la Mungu likiishi kupitia kwao. Mnaona? Jaribio huja kutikisa, kuweka kule chini kabisa, kuona mahali utakaposimama. Wao walijaribiwa, kumjaribu kila mwana amjiaye Mungu.

¹⁰¹ Ayubu alipitia katika majaribio na majaribu. Watoto wake wametwaliwa; kila kitu kinginecho kimechukuliwa. Wafuasi wa kanisa wakaja, wakamshtaki kuwa mwenye dhambi wa kisiri, na wakajaribu kusema kila kitu dhidi yake, bali asingesikiliza hata neno mojawapo. Yeye alijua ilikuwa ametimiza masharti ya Mungu. Alijua hakuna haja ya Shetani kujaribu kumjaribu. Alijua ilikuwa ni ibilisi. Na mradi tu Shetani anaweza kumfanya aamini ya kwamba ugonjwa wake unatokana na Mungu, amemshinda Ayubu. Bali mara Ayubu alipopata ufunuo huo, ya kwamba haikuwa ni Mungu! Yeye alikuwa anapitia tu kwenye

majaribio yake kumfanya kitu fulani. Si Mungu aliyekuwa anafanya jambo hilo. Ilikuwa ni Shetani aliyekuwa akilitenda.

¹⁰² Basi ni jambo lile lile leo. Atajaribu kukwambia majaribu haya na jambo hili ni Mungu wako akijaribu kukuadhibu. Sivyo ilivyo. La, bwana. Ni Shetani anayefanya jambo hilo, naye Mungu akiliruhusu, kukulainisha; kukufanya uone kama wewe u—umeshikwa na dunia hii, na masumbuko ya dunia, ama kama hazina zako ziko Mbinguni. “Kwa kuwa palipo na hazina yako, uko huko pia.” Hiyo ni kweli. Moyo wako uko penye hazina zako.

¹⁰³ Ayubu, alijaribiwa, hata hivyo akasema, “Najua Mkombozi wangu yu hai; kwenye siku ya mwisho Yeye atasimama juu ya nchi. Hata mabuu ya ngozi yangu yakiuharibu mwili wangu. . .”

¹⁰⁴ Mliona? Mabuu ya ngozi yalikuwa tayari yamo ndani yake. Mabuu ya ngozi yako yamo ndani yako. Wewe umo ndani ya sanduku lililofungwa bila hewa yo yote ndani yake, ama cho chote kile, bali mabuu ya ngozi tayari yako mle. Yamo ndani yako kabisa, nayo yako tayari kuitwa kazini wakati wote. Mkumbukeni Kaisari, yeye aliozea papo hapo barabarani. Mabuu ya ngozi yalimla, papo hapo barabarani, mabuu yake mwenyewe ya ngozi. Yako papo hapo, tayari.

¹⁰⁵ “Hata baada ya mabuu ya ngozi yangu kuuharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu.” Amina! Huwezi kuuangamiza kabisa. Hata mabuu ya ngozi yakiula, bado utarudi tena. “Ambaye nitamwona kwa nafsi yangu. Macho yangu yatamwona, na si mwingine.” Yeye alisema jambo hilo, Ayubu. Kwa nini? Yeye alikuwa mwamini. Katika majaribu alikuwa mwamini. Katika mateso, alikuwa mwamini. Alikuwa mwamini wa halisi.

¹⁰⁶ Yusufu, mwamini mwingine, asingejizua kuwa alivyokuwa. Alikuwa nabii. Mungu alimfanya nabii. Hakupenda kuwa tofauti na ndugu zake, lakini alikuwa tofauti. Mungu alimfanya alivyokuwa. Hakuna mtu mwingine angaliweza kupachukua mahali pake.

¹⁰⁷ Hakuna mtu anayeweza kupachukua mahali pako, haidhuru ni padogo namna gani. Unasema, “Mimi ni mke wa nyumbani tu.” Hakuna mtu anayeweza kupachukua mahali pako. Mungu, katika uchumi Wake mkuu, ameweka jambo hilo hivyo, Mwili wa Kristo, katika utaratibu, hata hapana mtu anayeweza kupachukua mahali pako. Jinsi gani ningalipenda kuchukua mahali pa Billy Graham, ye yote wetu wahudumu, lakini hatuwezi kufanya jambo hilo; bali, kumbuka tu, Billy hawezi kuchukua mahali petu. Mnaona, sote tuna mahali fulani, wengine wetu ni wainjilisti, wengine ni manabii, wengine ni walimu, wengine wachungaji, cho chote tulicho; wengine wake wa nyumbani, wengine ni makanika, wengine ni wakulima, cho chote kile, Mungu amekuweka katika mahali pako. Mnaona?

¹⁰⁸ Yusufu alikuwa nabii. Yeye asingejizua kwa sababu aliweza kufasiri ndoto. Hangeweza kujizua kwa sababu ya kwamba aliona maono. Angalia jinsi alivyokuwa mwaminifu. Haidhuru kama lilimgharimu ushirika wake na ndugu zake, alikuwa mwaminifu, kwa maana aliamini ndoto hizo. Yeye aliamini kwamba, ile ndoto aliyoota, ya kwamba wao wote wangemsujudu, ile miganda ingemsujudu. Ilitimia kwa maana yeye aliamini jambo hilo. Alikuwa mwamini halisi. Jinsi . . .

¹⁰⁹ Nina dakika tano; na kurasa kumi, angalia sasa, angalia, za Maandiko yaliyoandikwa hapa. Yule mwanamke . . .

¹¹⁰ Nathanieli, yeye alikuwa mwamini. Sivyo? Nathanieli, alipoona kilichotukia; nacho kikatenda kazi kwake, ya kwamba Yesu alimwambia yeye ni nani, naye akasema alikuwa “Mwi—Mwisraeli kwelikweli,” wala “hakukuwa na hila” ndani yake, na kumwambia mahali alipokuwa siku iliyotangulia, “akiomba chini ya mti.” Yeye alimwona wakati—wakati Filipo alipomwita. Alikuwa mwamini.

¹¹¹ Kuna wengi waliosimama pale, waliosema, “Hii ni roho ya ibilisi. Ibilisi anaponya Kiungu.” Ibilisi huyo wa kale hajafa bado leo. Wao wanaamini ya kwamba Ibilisi huponya Kiungu.

¹¹² Yesu alisema, “Kama Shetani anaweza kumtoa Shetani, basi ufalme wake umegawanyika, na ufalme huo hauwezi kusimama.” Unaona? Shetani alisema, katika . . . Yeye hawezi kufanya jambo hilo. Kwa hiyo, Shetani hawezi kumtoa Shetani.

¹¹³ Kwa hiyo Nathanieli alikuwa ni mwamini. Basi wakati alipoona Neno limefanyika mwili, likathibitisha kwamba yeye alikuwa ni mwamini, yeye alisema, “Wewe ni Rabi, Wewe ni Kristo. Wewe ni Mfalme wa Israeli.” Aliamini jambo hilo.

¹¹⁴ Wakati yule mwanamke kisimani alipoliona jambo hilo, aliliamini. Yeye ni mwamini.

Wakati kipofu Batimayo . . . Wakati mwanamke alipopita pale . . .

¹¹⁵ Na kila mtu alikuwa analia, akiendelea. Wengine wao wakisema, “Kuna mengi . . . Nasikia Wewe unawafufua wafu. Kuna uwanja mzima wa makaburi uliojaa hao hapa; njoo basi ukawafufue. Hebu tukuone ukifanya jambo hilo.” Mnaona, huyo ni ibilisi yule yule aliyesema, “Kama wewe ni Mwana wa Mungu, yaamuru mawe haya yawe mkate.” Mtu yule yule aliyemfunga kitambaa usoni Mwake, akampiga kichwani, kasema . . . wakapokezana fimbo, wao kwa wao, kasema, “Naam, kama utatwambia aliyekupiga, tutakuamini Wewe.” Hao askari, mnaona, wakimfanyia dhihaka. Ilionekana kana kwamba mambo yamemwendea kombo, Yeye.

¹¹⁶ Lakini hebu kumbuka tu, Mungu daima yuko uwanjani. Mnaona? Yeye yuko pale pale akiwa tayari, wakati wo wote.

117 Sasa Yesu alisema, “Ningeweza kuzungumza na Baba Yangu na mara moja angenipelekea makundi kumi na mawili ya Malaika.” Loo, Malaika mmoja angefanya nini? Mnaona? Lakini, unaona, bali Yeye angeweza kutuma makundi kumi na mawili kwa amri Yake tu. Bali Yeye alikuwa na kazi ya kufanya. Alikuwa na kazi ya kufanya. Ilimbidi kupitia jambo hilo.

118 Unalo jambo la kufanya. Mungu ana jambo kwako wewe la kufanya. Huenda ukawa na majonzi na shida fulani, huenda ukakosa utakacho, lakini sisi huomba tuziepuke? La. “Bwana, nipitishe katika hayo, hata yawe nini. Hata iwe ni nini, usiniache kuyaepa. Kama yamewekwa kwa ajili yangu, nipe tu neema ya kupitia hayo. Hivyo tu.”

119 Sasa angalia, kipofu Batimayo, yeye alijua jambo hilo. Wao waliambiwa, “Huyu ni yule Nabii wa Galilaya. Yeye ni Mwana wa Daudi. Tunaamini jambo hilo.” Baadhi ya waamini hawana budi walimwambia jambo hilo. “Sisi waamini tunajua ya kwamba Yeye ni . . . yule Mwana wa Daudi.”

120 Naye alijua, kama Yeye alikuwa, Yeye alikuwa Neno. Na kama alijua alikuwa Neno, alijua angaliweza kuyatambua mawazo ya moyo, kwa hiyo alipaza sauti, “Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu.” Wasioamini walikuwa wanapiga makelele *hivi*, na *vile*, washiriki wa kanisa. Jambo hilo halikumzuia kipofu Batimayo kamwe. Akasema, “Ee Yesu, Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu!”

121 Labda asingeweza kumsikia. Bali Yeye alijua alikuwa anapaza sauti, ndipo akasimama akageuka. Huyu hapo mwamini. Yeye alisema, “Imani yako imekuokoa.” Amina.

122 Alimwambia hivyo mwanamke aliyetokwa na damu, jambo lile lile, “Imani yako.”

123 Maana, yeye alisema ndani ya moyo wake, “Kama naweza kugusa vazi Lake, nitapata afya.”

“Imani yako imekuokoa.” Mnaona, yeye alikuwa mwamini. [Ndugu Branham anapigapiga mimbara mara kadha—Mh.]

124 Hilo ndilo jambo lile lile lililomwoko William Dauch, anayeketi pale, juzijuzi, akiwa na kukoma kabisa kwa moyo, na ugonjwa mbaya wa moyo, mtu mwenye umri wa miaka tisini na moja. “Imani yako imekuokoa.” Kwa nini? Yeye ni mwamini.

125 Kasisi Tom Kidd hapa, hata kwenda kwenye nini-hii yake. . . karibu, nadhani, karibu kabisa na umri wa miaka tisini sasa, mzee, karibu na huo. Na wakati alipokuwa na umri wa miaka sabini na tisa, wao walimpeleka hospitalini akiwa na kansa kwenye kibofu chake. Daktari anasema, “Hawezi kupona.”

126 Bali wakati tulipoingia asubuhi ile, tukamwona maskini mzee huyo wetu akiwa na shali mabegani mwake, ameketi pale, akitikisa fimbo ndogo, alikuwa karibu amerukwa na

akili. Akamwambia mwanamke kizee aliyekuwa ameketi pale, alimwita nyanya; alimjua, mmoja wa wafuasi wake kwa miaka kadha. Kasema, “Unaonekana mweupe kama theluji,” amerukwa na akili.

¹²⁷ Hata hivyo, Nguvu za Mungu zilipoingia chumbani, yeye yu hai usiku wa leo. Hiyo imekuwa miaka minne iliyopita. Mtu mwenye umri wa karibu miaka thamanini, naye huyu hapa ameketi usiku wa leo, akiwa mzima kabisa na mwenye afya, kutokana na kansa. Mnaona, si mwamini wa kujifanya; mwamini! Jambo ndilo hilo, amini! Yeye analiamini Neno Lake Mungu.

¹²⁸ Ni vile vile tu kipofu Batimayo alivyokuwa. Kipofu, bali hata hivyo yeye alijua, kama angaliweza kuuvutia usikivu wa Yesu Kristo, angalipata alichotaka.

¹²⁹ Yule mwanamke alijua, kama angaliweza kugusa vazi Lake, angepata kile alichohitaji—angepata alichohitaji.

¹³⁰ Tom alijua. Alikuwa na imani, kama ningemwombea, angepata alichohitaji.

¹³¹ Hivi hiyo siyo imani ile ile ambayo Martha alisema? “Hata sasa, Bwana, yo yote utakayomwomba Mungu, Mungu atakufanyia. Ndugu yangu amelala kule, amekufa, siku nne kaburini; lakini Wewe mwombe tu Mungu, Naye Mungu atakutendea jambo Hilo.”

Kasema, “Ndugu yako atafufuka tena.”

¹³² Naye akasema, “Naam, Bwana, katika siku za mwisho, katika ule ufufuo, yeye atafufuka. Alikuwa mvulana mzuri.”

Yeye akasema, “Lakini Mimi ndiye huo ufufuo na Uzima!”

“Naam, Bwana, ninaamini jambo hilo, pia.”

“Mlimzika wapi?” Haya basi. Imekwisha. Naam, bwana.

¹³³ Malkia wa Kusini alikuja katika kizazi hicho cha wasioamini, hiyo ni kweli, kisha akasimama pale na kuamini kile alichoonza kwamba ni cha Mungu. Biblia ilisema, “Yeye atasimama katika siku ya mwisho, pamoja na kizazi hicho, na kukihukumu, kwa maana alitoka kutoka pande za mbali za dunia kusikia hekima ya Sulemani.”

¹³⁴ Musa alikuwa mwamini. Ingawa alijaribu kiakili, alikuwa amejaribu kila mbinu aliyoweza, bali isingefanikiwa. Alijaribu kuwatoa Israeli, alijua kwamba aliitwa kufanya jambo hilo. Alijaribu kwa njia ya hesabu. Alijaribu kijeshi. Alijaribu kielimu. Alijaribu kila njia, bali haingefanikiwa. Lakini baadaye akachukua njia ya Mungu.

¹³⁵ Kulitukia nini? Kulikuweco na Moto kijitini kule, siku moja, ambao usingeondoka. Kutoka kule Neno likanena naye, likasema, “MIMI NIKO.” Si, “Nilikuwa, wala, Nitakuwa.”

“MIMI NIKO.” Naye yungali yule “MIMI NIKO.” Yeye ni Neno, la Milele, Neno la milele.

¹³⁶ Musa hakutilia shaka. Shida nyingi dhidi yake, kila maumbile yanampinga, kila kitu kinampinga. Lakini, huku ameshika fimbo iliopindika mkononi mwake, alishuka akaenda akaliteka taifa zima, na kulizamisha katika Bahari ya Chumvi kule nje, kisha akawachukua Israeli kwenye nchi ya ahadi. Kwa nini? Yeye alimwamini Mungu. Sawa. Alikuwa na . . .

¹³⁷ Huyu ni mwamini. Tungeveza kukaa . . . Sasa nimetumia nusu saa yangu juu ya waamini.

¹³⁸ Nina tabaka nyingine mbili. Tutaharakisha tuwamalize, maana hao si muhimu, hata hivyo. La.

¹³⁹ Halafu, pili, anakuja sasa asiyeamini. Hebu sasa tuzungumze juu ya asiyeamini naye. Asiyeamini hufanya nini?

¹⁴⁰ Tunamwona mwamini (ati nini?) hulikubali Neno; kila jamii, kila kizazi, tangu wakati wa Nuhu, kuendelea mbele. Tungechukua miezi sita ya ufufuo moja kwa moja juu ya jambo hilo hapo, tukiwasimulia hao watu. Wao wanaamini. Mwamini haulizi. Mwamini huliadini Hilo, haidhuru linasikika namna gani ama lo lote mtu ye yote asemalo juu Yake, jinsi linavyoonekana lisilowezekana.

¹⁴¹ Mwamini huliadini, anaamini (kitu gani?) Neno. Si kanuni za imani; Neno! Si madhehebu; Neno! Si kile anachosema mtu mwingine; kile lisemacho Neno! Naam, kumbukeni, huyo ni mwamini. Mwamini haulizi. Mwamini hasemi, “Inawezekanaje? Laiti ningaliweza kulielezea!” Huyu ni asiyeamini. A-ha. Ni mwamini, ambaye, haidhuru ni kitu gani, “Kama ni Neno, Ni Neno! Hilo ni kweli.” Huyu ndiye mwamini.

¹⁴² Sasa asiyeamini. Sasa tunaona vile . . . Tutawachukua wasioamini. Tunaona ya kwamba wao waliendelea vema mradi tu wao wanapongezwa na kuitwa wanafunzi. Mradi tu (wao) kila kitu kilienda shwari, walikuwa shwari. Bali wakati Nabii huyu ambaye waliadini alikuwa nabii fulani, nao walijua alikuwa nabii, ambaye aliweza kuwaponya wagonjwa, na kadhalika, Yeye alifanya kitu gani? Wakati ile kweli halisi na lawama zilipokuja, kinyume na yale waliyoamini, wao hawakuweza kulistahimili Neno.

¹⁴³ Waliweza kukubaliana na miujiza, nao waliifanya. Walitoka wakaenda na kutoa pepo, wakahubiri Neno, na wangali wasioamini. Mathayo 10, Yeye aliwatuma, wawili wawili, wale sabini, nao wakawatoa pepo, hata kwamba Yesu akafurahi, na kusema, “Nilimwona shetani akianguka kama nuru kutoka Mbinguni.” Unaona, wao walitoa pepo; Yuda akiwa papo hapo pamoja nao. Hawa hapa wasioamini wanakuja.

¹⁴⁴ Lakini mara Yesu alipoanza kusema ya kwamba Yeye alikuwa kitu fulani, ya kwamba Yeye alikuwa ni “ufufuo,” Yeye

alikuwa “Uzima.” “Mngesemaje kama mkimwona Mwana wa Adamu akipaa kutoka mahali lipotoka?”

¹⁴⁵ “Naam, Mtu huyu anajaribu kusema amekuja kutoka Mbinguni, hilo limezidi sana kwetu. Hatuwezi kuamini jambo Hilo.”

¹⁴⁶ Akasema, “Ni nini? Huo mwili ambao mnazungumzia habari zake, haufai kitu. Roho ndiyo itiayo uzima.”

¹⁴⁷ Hapo basi. Roho hulihuisha Neno. Ni Roho, si kanuni za imani. Roho, wa Roho Mtakatifu, hulihuisha Neno kwako, nalo linakuwa hai, na hapo basi, unaliona. Kwa imani unaliona. Unajua ni hivyo kwa sababu Neno lilisema hivyo, naye Roho analihuisha Neno kwako. Haya basi.

¹⁴⁸ Sasa Yeye alisema, “Mta-...” Na mara tulipofanya jambo hili, tunaona, wasioamini, unaposema jambo wasilokubaliana nalo, wanakuacha wanaenda zao. “Mimi nakataa!” Loo, hilo linakuwa lenye kilindi sana, katika ulimwengu leo. Anza na useme tu kitu fulani...

¹⁴⁹ Wanakusanyika. Ninaona kwenye mikutano watakusanyika, halaiki ya watu, nawe unasimama, unaanza kusema jambo fulani. Naam, mradi...Naye ataketi pale, akiangalia tu, akingojea tu. Ndipo mara unaposema, “Naam, Yesu Kristo alijitambulisha kama Masihi, kwa maana Yeye alikuwa ni Nabii,” kopo hilo tayari limejaa, linaondoka linaenda zake. Mtu fulani...nao wanaondoka wanaenda zao. Ni kitu gani? Wasioamini!

¹⁵⁰ Sasa mnasema, “Unajitungia hilo.” Sijitungii. Ninasema kile hasa Biblia inachosema hapa.

¹⁵¹ Wao walikuwa wasioamini, nao wakaondoka. Ingawa walikuwa wanafunzi, bali ilikuwa ni—ni kinyume na yale... Walisema, “Hili, ni nani angeamini jambo kama Hilo?” Mnaona? Wao walikuwa ni Mafarisayo na Masadukayo waliokuwa wametoka, wakajiunga na kuambatana Naye.

¹⁵² Kwa maana, mnaona, wakati yale—yale ya kimbinguni yakionyeshwa wazi, hutoa aina tatu tofauti. Yalifanya jambo hilo kule Misri. Yalitoa asiyeamini, mwamini, na mwamini wa kujifanya. Yalitoa tabaka zote tatu. Nimeziandika tu hapa chini, hata tunaendelea tu na kuendelea usiku kucha, tukizielezea, jinsi mambo yalivyo. Kila mahali, unalipata jambo hilo, mnawaona hao watatu. Ndivyo ilivyo daima, mnaona, mnawapata.

¹⁵³ Sasa angalia, hawa sabini, walitoka wakaenda kwa sababu Hilo halikukubaliana na yale waliyoamini kuwa ni ya kweli.

¹⁵⁴ Hatuna wazo linalokuja. Ni yale aliyosema Yeye! Unakana mawazo yako mwenyewe. Unasema tu analosema. Huko ni kuungama kweli. *Kuungama* kunamaanisha “kusema jambo lile lile.” Kama niliungama kwamba jambo fulani lilitukia,

ninasema jambo lile lile lilitotukia. Huko ndiko kuungama halisi. “Naye ni Kuhani Mkuu wa maungamo Yetu.” Unaona? Kusema jambo lile lile alilosema Mungu, mnaona, hilo hulifanya sahihi, maana wewe unarudia tu Neno la Mungu.

¹⁵⁵ Sasa angalia, wale sabini waliondoka wakaenda zao. Walifanya nini? Nao—wao walienda zao kwa sababu tu ha—hawakukubaliana. Hekima ya—ya—yao, kujiunga kwa—kwao na kanisa kulikuwa, ku—kulizidi sana. Hilo lilikuwa ni zito mno kwa wao kuwazia, ya kwamba Mtu huyu anayesimama hapa, kwamba nini-hii... Watu wengine wote waliamini kwamba Huyu alizaliwa haramu. “Hakuwa na haki ya kujiita Mwenyewe Mungu. Naye alikuwa mwanadamu tu.” Kasema, “Hatukupigi Wewe mawe kwa kazi nzuri ufanyayo, lakini tu—tunakupiga mawe kwa kuwa Wewe, ukiwa Mwanadamu, wajifanya Mwenyewe Mungu.”

¹⁵⁶ Nalo Neno lilisema Yeye alikuwa ni Mungu. “Ataitwa Jina Lake ‘Mshauri,’ ‘Mfalme wa Amani,’ ‘Mungu Mwenye Nguvu,’ ‘Baba wa Milele,’” Maandiko yao yale yale yaliyosoma!

¹⁵⁷ Na siku ile ile wao waliyokuwa wanaimba Zaburi, Zaburi 22, “Mungu Wangu, Mungu Wangu, mbona umeniacha? Mifupa Yangu yote inanikodolea macho.” “Hakuna hata mfupa mmoja utakaovunjwa.” Wimbo ule ule waliokuwa wanaurudia hekaluni, huyo hapo yule Dhabihu ametundikwa akiyanena maneno yale yale kwa sauti kuu ambayo Daudi aliyasema miaka mia nane hapo kabla, nao walikuwa vipofu sana kuona jambo hilo.

¹⁵⁸ Na, leo, Mungu yule yule ambaye alinena habari za wakati huu amejitokeza akifanya vile vile kabisa Yeye alivyosema angefanya, nao ni vipofu sana hawawezi kuliona. Hao ni wasioamini. Wao wanaondoka wanaenda zao na kusema, “Loo, siwezi kuamini upuzi kama Huo. Sijasikia hilo maishani mwangu!” Haijalishi ulisikia nini. Biblia ilisema lingekuwa hapa, na ni Neno Lake.

¹⁵⁹ Hawakuwa kamwe wamesikia jambo Hilo, pia, bali lilikuwepo tu pale haidhuru. Mnaona? Hiyo ni kweli. Walikuwa wasioamini.

¹⁶⁰ Kama tu Hawa alivyokuwa, alikuwa ni wa kidini sana, bila shaka, kwa hiyo, lakini yeye—yeye hakuamini Neno la kweli. Naye ilimbidi kujifanyia dini, kwa hiyo akajitengenezea majani ya mtini, mnaona, bali jambo hilo lisingefaa. *Dini* maana yake ni “kifuniko.”

¹⁶¹ Kaini alifanya jambo lile lile. Kaini hakuweza kuamini kwamba Jambo Hilo lilikuwa sawa. Alisema, “Mungu ni mtakatifu, Mungu ni msafi, na Mungu ni mzuri. Kwa hiyo nitajitafutia maua, nami nitachukua ma—maua na nitatengeneza madhabahu nzuri na kubwa, kisha nita—nitamwonyesha Yeye kicho changu. Nitaondoka nisimame mbele

yake, kisha nitasujudu mbele Zake na kumwabudu Mungu huyo. Nami nitaweka maua kwenye madhabahu, kwa maana, mwajua, baba yangu na mama yangu walikula matofaa fulani, matunda fulani, kwenye bustani ya Edeni, na jambo hilo ndilo lililonileta. Na kwa hiyo, hiyo ni kusema, nitarudi, maana nitaifanya kuwa ya kupendeza. Mungu hawezi tu kulikataa kanisa langu kuu. Naam, nitakuwa kanisa kubwa mno! Nitalifanya zuri sana hata litauvutia usikivu wa Mungu.” Shetani ndiye anayekaa katika urembo. Hivyo ndivyo Maandiko yanavyosema hasa.

¹⁶² Hiyo ndiyo sababu, wakati mwingine, mwanamke mrembo ni chambo cha Shetani. Kama anaweza tu kumshika, anaweza kuwafingirisha wanaume wengi zaidi jehanamu kuliko vile angeweza kufanya na baa zote nchini. Hiyo ni kweli. Mnaona? Ama, mzuri, mwanamume fulani mkubwa mno mwenye sura nzuri ambaye asinge—asingelisimama katika uhalisi wake wa utu uzima, mnaona, tena, anaweza kuwafingirisha hao wanawake kwa ibilisi, na kuwapeleka jehanamu. Naam, bwana.

¹⁶³ Angalia, Shetani anaishi katika urembo. Alijaribu kufanya nini hapo mwanzo? Kufanya ufalme mzuri sana kuliko wa Mikaeli ulivyokuwa; akaondoka akaenda Kaskazini, na kuchukua theluthi mbili ya Malaika pamoja naye.

¹⁶⁴ Mnaona ni wa nani—huyo alikuwa mwana wa nani basi, aliyekuwa na tabia hiyo ndani yake? Mwana wa Shetani. Bila shaka, hakika ndivyo alivyokuwa. Basi alijenga madhabahu, kisha akapiga magoti na kuabudu. Alipitia kila kitu ambacho (Kaini) abacho Habili alitenda.

¹⁶⁵ Lakini Habili alijua kwamba sivyo ilivyokuwa. Yeye... Damu ndiyo iliyowatoa. Alijua kwamba ilikuwa ndiyo yenyewe. Ilikuwa ni kujuana kimwili, damu. Kwa hiyo akachukua mnyama mdogo, na kumtoa dhabihu mwambani, akamkata shingo.

¹⁶⁶ Mwangalie Kaini, yeye... Mungu alimwambia, akasema, “Mbona usiabudu kama ndugu yako, nawe utafanya vyema. Utafanya vyema kama ukifanya jambo hilo.” Lakini, la, yeye alijua mengi mno juu ya jambo hilo. Mnaona, yeye alikataa la asili, Neno lililothibitishwa. Kama hao sio watoto wake leo! Mnaona?

¹⁶⁷ Sasa angalia, “Mungu alishuhudia,” Biblia ilisema. Waebrania sura ya 4, ama sura ya 11, “Mungu akishuhudia kipawa Chake, kwamba alikuwa mwenye haki.” Mungu alithibitisha dhabihu yake. Mungu alithibitisha ya kwamba jambo hilo ndilo alilokubali; hilo lilikuwa Neno Lake, mpango Wake.

¹⁶⁸ Ndipo akamwambia Kaini, kasema, “Fanya jambo lile lile, nawe uishi.” Lakini mnafikiri yeye angeacha, yeye angeacha wazo lake? La, bwana. Yeye alikuwa asiyeamini, naye akaondoka akaenda zake moja kwa moja. Hiyo ni kweli. Kaini alifanya

jambo lile lile. Nimrodi alifanya jambo lile lile. Wasioamini! Yeye hakuamini.

Belteshaza, jambo lile lile, hata hivyo, ama . . .

¹⁶⁹ Nebkadreza, ingawa alikuwa amemfanya Danieli kama mungu wake, akamwita Belteshaza, ambalo lilikuwa ndilo jina la mungu wake, alimwona Danieli akifanya kazi kuu za Mungu. Na ndipo akajua ya kwamba—ya kwamba Belteshaza aliamini, ama Danieli alikuwa mungu, kwa hiyo akafanya sanamu yake, na kuiweka kule nje na kufanya kila mtu aiabudu, na kadhalika. Mnaona, ufalme wa Mataifa ulianza kwa kulazimisha kuabudiwa kwa sanamu ya mtu mtakatifu, na ufalme wa Mataifa unaishia kwa kulazimisha sanamu ya mtu mtakatifu, mnaona, namna ile ile.

¹⁷⁰ Na kulikuwako na maandiko kwenye ukuta, ya lugha isiyojulikana, hapo mwanzoni mwa ufalme wa Kimataifa, ambayo hakuna mtu angaliweza kuyasoma ila nabii huyo. Pia kuna maandiko kwenye ukuta leo, hiyo ni kweli, “Ichabod,” ya kwamba utukufu wa Mungu umeondoka kwenye mambo hayo. [Ndugu Branham anapiga makofi, mara mbili—Mh.] Nayo maandiko yako kwenye ukuta na yanaweza kusomwa na mtu wa kiroho anayeamini katika mambo ya kiroho, aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu.

¹⁷¹ Mzee Belteshaza anaondoka anaenda na kuchukua vyombo hivi vya Bwana, kunywa mvinyo navyo. Kwa nini? Yeye alikuwa asiyeamini. Alifikiri alikuwa mwamini, bali alikuwa asiyeamini. Mnaona, naam, yeye alikosa kuliadini Neno.

¹⁷² Ahabu, yeye alikuwa asiyeamini, ingawa ali—alitenda kama kwamba hakuwa. La, la, yeye alikuwa kati ya waamini, bali alikuwa asiyeamini. Alifanya nini? Alimwoa mwabudu sanamu, kisha akaileta, ibada ya sanamu, moja kwa moja katika Israeli. Alikuwa asiyeamini. Tunajua jambo hilo.

¹⁷³ Wao wanakataa Neno lote la Mungu kuwa ni kweli. Asiyeamini ni, mnaona, sasa kumbukeni, yeye ni mnafiki. Naye ana—anatenda namna hiyo, anasema analiamini Hilo, bali analikataa. Yeye alisema, “Vema, sehemu Yake kiasi ni sawa.” Bali kama lote si kweli, basi hilo linamfanya asiyeamini. Huna budi kuamini kila nukta na kila yodi, na kila kitu kilichosemwa Humo ndani. Hakina budi kuwa ni kweli. Kama si kweli, kama ukisema sasa, “siamini jambo Hilo,” vema, basi wewe ni asiyeamini.

¹⁷⁴ Kuna jamaa aliyeniambia, wakati mmoja, m—mhudumu alisema, “Sijali, Bw. Branham, ni watu wangapi ungeweza kutoa ambao—ambao ulisema waliponywa, nisingeamini jambo hilo.”

¹⁷⁵ Nikasema, “La bila shaka, huwezi kuamini jambo hilo. Wewe ni asiyeamini. Halikuwa kwa ajili yako. Ni kwa ajili ya waamini pekee.”

¹⁷⁶ Huna budi kuamini jambo hilo. Unaona? Nao hawaliadini. Kwa hiyo unapomwona mtu ambaye, Paulo alinena vema juu ya manabii, akisema kwamba wao wangekuwa “wenye vichwa vigumu, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu; wenye mfano wa utauwa, bali wakizikana Nguvu pale, Nguvu za Neno; hao nao ujiepushe nao.” Angalia, wao wanakana Neno lote, bali wao ni wa dini katika kila hali. Wao ni wasioamini katika Neno la kweli, hata lithibitishwe.

¹⁷⁷ Sikuzote katika kila wakati, Mungu alithibitisha Neno la watu hawa niliozungumza habari zao, Nuhu, na kuendelea kupitia kwa Musa, na manabii wote, na kadhalika. Mungu alinena kwa mambo ya kimbinguni na Neno lililothibitishwa, na hata hivyo watu hao walijitenga nalo papo hapo.

¹⁷⁸ Na hapa wapo hawa wanafunzi wamesimama pale, hao sabini, huku wakimwagalia Yesu akifanya mambo yale aliyoyafanya, na kuyajua Maandiko, Naye akiwaambia ya kwamba huo ndio wakati ambao jambo hili lilipaswa kutukia. Halafu basi wakati Yeye aliposema jambo fulani, “Mwana wa Adamu, mnasemaje...” Wakati alipoanza kuwaambia juu ya kuumega mkate, na kadhalika, na akaendelea kuwaambia juu ya mambo makuu ya kiroho.

Nao wakasema, “Loo, Hili ni neno gumu!”

¹⁷⁹ Yeye alisema, “Mtasemaje basi kama, Mwana wa Adamu, mkimwona akipaa juu Mbinguni alikotoka?” Kasema, “Ni mwili, ama ni Roho, inayohuisha?” Mnaona?

¹⁸⁰ Kisha wakaondoka, kasema, “Loo, Hilo, la, siwezi kuamini jambo Hilo.” Mnaona? Wakaondoka moja kwa moja, kwenye Neno. Wao hata hawatakaa kuona linalotukia. Huyu ni—huyu ni asiyeamini.

¹⁸¹ Wao, wanafanya nini basi? Tunaona ya kwamba wao, ya kwamba watu hawa, hawa waamini, wanaoitwa waamini, bali katika mifano ya dini, nao wanashindwa kuona Kweli iliyotambulishwa ya Neno la Mungu kwa maana inapingana na wanayoamini. Mnaona?

¹⁸² Haileti tofauti yo yote unaloamini, jinsi ulivyo mnyofu, jinsi ulivyo wa dini, ama, hilo halina uhusiano wo wote na jambo hilo. Unyofu, mbona, hilo halina uhusiano wo wote nalo. Nimeona watu wanyofu sana! Nimeona makafiri wakiwachoma moto watoto wao, wakiwalisha mamba, mama wakiwa na watoto wao wachanga. Hilo ni zaidi ya vile Mkristo angalitenda. Mnaona? Kwa unyofu wanaamini, kwa unyofu, bali wao walikuwa wanyofu kimakosa.

¹⁸³ Watu wanasema, “Vema, kanisa hili limedumu!” Hilo, u mnyofu kimakosa, kama liko kinyume na Neno. “Vema, sasa angalia, siamini jambo kama hilo!” Ambapo, Biblia imesema Jambo hilo ni la kweli, kwa vyo vyote! Mnaona? “Siamini

kwamba inatubidi kufanya jambo *Hili*.” Sijali unalofikiria wewe haikubidi kufanya. Mungu alisema halina budi kufanywa.

¹⁸⁴ “Ishara hizi zitafuatana na hao.” Mpaka wapi? “Kote ulimwenguni.” Akina nani? “Kwa kila kiumbe.” Unaona, itakuwa; “si itakuwa?” Itatendeka!

¹⁸⁵ Basi Ujumbe huu wa wakati ambao tunaufurahia sasa, Uwepo wa Mungu, siku za baadaye, wakati wa jioni wakati Nuru zinawaka, na mambo yale ambayo yamefunguliwa, na Neno kuthibitishwa na kuhakikishwa kuwa ni Kweli; pia yametabiriwa, yanatukia, kwa kisayansi na kila kitu, vilithibitishwa ya kwamba Hilo ni, “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.” Na, mtu analikimbia jambo Hilo, yeye—yeye ni asiyeamini. Hana matumaini. Yeye ametiwa ganzi na nguvu za Shetani, kwa hiyo hakuna matumaini kwake. Hana matumaini kabisa.

¹⁸⁶ Sasa jambo hilo ni nini? Mwamini; sasa asiyeamini; sasa tabaka ya tatu, tunayezungumza habari zake, ni mwamini wa kujifanya. Huyu ndiye mwenyewe, mwamini wa kujifanya! Naam, kumbukeni, hapo ndani walisimama wote watatu. Naam, tunaona sasa, wao wanafanya sawa kabisa kama baba yao afanyavyo, Yuda.

Kulikuweko na Petro na mitume wengine, waamini.

Kulikuweko na wale sabini, wasioamini.

¹⁸⁷ Kisha kulikuweko na Yuda, aliendelea kusitasita, alikuwa mwamini wa kujifanya. Wao wanafanya nini? Hawa ni wale wanaositasita mpaka wanapoweza kupata jambo fulani, kosa ndani Yake. Wao daima wanatafuta kupata mwanya, kuona jinsi linavyotendwa, kuona kama ni ujanja, kama ni kiinimacho. Wao wanagoeja kuuzwa. Wanatazamia jambo hilo.

¹⁸⁸ Asiyeamini, yeye hata hangojei. Amekwisha kulihukumu, na akaenda zake.

¹⁸⁹ Mwamini, haidhuru nini kinachotukia, analiamini, haidhuru, kwa kuwa ni Neno.

Hizo hapo takaba zako tatu.

¹⁹⁰ Maskini asiyeamini atatoka aende zake, kwa jambo la kwanza lililosemwa, hataki kitu kuhusu jambo hilo. Ndugu, yeye ataonyesha jinsi alivyo papo hapo. Yeye ni asiyeamini. Paulo alisema, “Walitoka kwetu, kwa maana hawakuwa wetu, tangu mwanzo. Walianza pamoja nasi.” “Loo, mlikimbia vizuri; ni kitu gani kiliwazuia?” Mnaliona? “Wao walitoka wakaenda zao, kwa kuwa hawakuwa wetu.” Wanapoliona Neno likiendelea moja kwa moja kikamilifu, mbona, wao walitaka kupata namna fulani ya kiinimacho wangaliweza kufanya. Mnaona?

¹⁹¹ Bali waamini halisi hawaulizi kitu. Imeandikwa katika Neno, nao wanaliamini, nao wanaendelea tu. Hilo, hivyo ndivyo ilivyo. Daima, imeandikwa. Kama haikuandikwa, mbona,

usilikaribie, haidhuru nini kitukie. Haina budi kuandikwa. Unaona? Nao wanaona hilo neno lililoandikwa na wanaliadini. Nao wanamwona Mungu akitenda katika Neno Lake, wanaona ile saa, ule Ujumbe, ule wakati, nao wanatembea pamoja Nalo.

¹⁹² Kama nilivyosema asubuhi ya leo, jinsi maskini Pilato ilivyombidi kutembeatembea sakafuni, usiku, akiwa na dhamiri yake iliyokuwa na hofu, akijaribu kujisafisha. Naye akasema, jamani, wakati hapana shaka alikuwa ameita usiku kucha, kasema, “Ni—ni—nime—nimenawa mikono yangu, usiku kucha, na bado siwezi kuelewa. Mnaona, si misafi. Siwezi kwenda kukutana Naye kamwe; nina Damu mikononi mwangu.” Loo, jamani! Unaona, usiwe na hatia ya jambo hilo kamwe. Unaona?

¹⁹³ Iko mikononi mwako. Kuna njia moja tu unayoweza kuiondoa; nayo ni, kuikubali, hiyo ni kweli, kuwa sehemu Yake. Ilimwagwa kwa ajili hiyo.

¹⁹⁴ Naam, mwamini wa kujifanya anaendelea na kujifanya mtawa kama awezavyo, lakini ndani ya moyo wake anajaribu kupata jinsi—jinsi, wewe, jinsi unavyofanya jambo hilo. Loo, kama nchi haikujaa sehemu hiyo, ya wanafiki! Naam. Huyu ni Yuda. Hiyo ni kweli kabisa. Anaendelea, anakuwa sehemu ya kundi; alikuwa mweka hazina, mnaona. Yeye husimama karibu, daima ameinyosha mikono yake apate pesa. Unaweza kujua jambo hilo, jambo moja, daima anatafuta-tafuta pesa, naye amenyosha mikono yake azipate. Naye ni mwamini wa kujifanya. Anatenda kama mwamini, bali ndani ya moyo wake...

¹⁹⁵ Kumbukeni, hakuwa akimdanganya Yesu. Baada ya wale sabini kuondoka, na hawa waamini wakachukua msimamo wao; basi Yeye akawageukia waamini, akasema, “Kungali kuna jambo fulani ndani yenu,” kwa kuwa alisema, “Nimewachangua kumi na wawili, na mmoja wenu ni ibilisi.” Yesu alijua, tangu mwanzo, kwa kuwa alikuwa Neno. Yeye alijua siri ya moyo.

¹⁹⁶ Jinsi lilivyokuwa jambo gumu! Simama kidogo. Tafakarini sana, kwa muda mrefu, sawasawa! Jinsi hapana budi hilo lilikuwa jambo gumu sana Kwake, akitembea papo hapo, na mtu fulani akimwita Yeye, “Ndugu,” huku anajua wakati wote ya kwamba huyo alikuwa ndiye huyo mdanganyifu atakayejaribu kumfadhaisa, na kumuza kwa vipande thelathini vya fedha. Jinsi lilivyokuwa gumu kulishikilia moyoni Mwake, huku rafiki Yake anatembea pale. Hata yeye alisema, “Rafiki,” alimwita Yuda rafiki Yake, “je! mimi sijakuwa pamoja nawe, wakati huu wote?” Akijua ndani ya moyo Wake, naye hakuweza kulisema jambo hilo. Yeye alijua, tangu mwanzo, ni nani atakayemsaliti.

¹⁹⁷ Huyu hapo yule mwamini wa kujifanya ambaye anangojea tu. Yeye ataimba jambo hilo, aseme, “Loo, ninaamini jambo *hili*, pia ninaamini jambo *hili*, na ninaamini *hili*. Lakini, loo, mwajua,

nilimsikia mtu fulani akisema ni mara *kadha wa kadha*.” Loo, mnaona, maskio marefu tu.

¹⁹⁸ Mwamini halisi hasikii kitu ila Neno. Hakuna zaidi. Yeye huliangalia Neno. Hatafuti mianya. Yeye hatafuti viinimacho. Anamwamini Mungu, na hilo latosha, naye anaendelea tu. Mnaona? Huyo hapo mwamini.

¹⁹⁹ Asiyeamini hujaa kwa dakika moja, wala hawezi kuketi kusikiliza dakika kumi za Ujumbe. Hana budi kuamka aende zake. Ni kinyume cha kanuni ya imani yake, wala hatakuwa na uhusiano wo wote nalo, kwa hiyo anatoka.

²⁰⁰ Halafu, mwamini wa kujifanya anaendelea tu, huyo Yuda. Mnaona, huyo ndiye madanganyifu. Huyo ndiye—ndiye mlaghai, kama itanibidi kusema neno kama hilo. Yuda, yeye anasitasita. Huu ndio wakati, mara kwa mara, hawa waamini wa kujifanya hupendwa sana na watu. Hiyo ni kweli, hawa waamini wa kujifanya, mnaona. Wengine wao ni watu wakuu sana, wenye elimu, digrii ya udaktari, mshahara mkubwa, kila kitu. Wengine wao ni watu mashuhuri, werevu, kama tu ambavyo wangekuwa wana wa Shetani.

²⁰¹ Angalia jinsi Shetani alivyokuja moja kwa moja kule na kukubaliana na kila kipengele cha hilo Neno; yeye angokea tu kupata sehemu hiyo nyonge kwa Hawa, ambapo angeonyesha nguvu zake za kumdanganya, kumsaliti. Huyo alikuwa—huyo alikuwa Shetani. Basi huyu hapa Shetani, katika mfano wa Yuda, katika wakati ule. Huyo alikuwa ni Shetani katika ule wakati wa kwanza. Alikuwa nini? Akikubaliana na Neno mpaka akafikia kwenye jambo moja dogo; anajaribu kutafuta mahali anapoweza kupata udhaifu.

²⁰² Basi hilo ndilo hasa analopata Yuda sasa hivi. Ataifuatilia mkutano moja kwa moja, aangalie kila mahali mpaka anapoweza kupata sehemu hiyo ndogo ambayo, yeye, “Loo, hiyo hapo! Haya basi!” Unaona? “Loo, kumbe hivyo ndivyo inavyofanywa!” Unaona? Ndivyo hasa.

²⁰³ Wengi wenu mnakumbuka kule juu usiku ule wakati mtu yule alipokuja jukwaani. Yeye alidhani kwamba kulikuweco na uwezo wa kushirikiana mawazo katika kusoma kadi za maombi, na jinsi alivyodhani kwamba amelipata papo hapo. Ndugu, yeye—yeye alikuwa na uhakika alikuwa amelipata. Ndipo akasogea karibu. Alikuwa mfuasi wa kanisa ambalo haliamini katika—katika—katika mambo haya, katika Injili, Injili yote. Ndipo akapanda akaja jukwaani. Nilikuwa nimechoka. Walikuwa wanajitayarisha kunichukua.

²⁰⁴ Hiyo ilikuwa huko Windsor, Ontario. Mle ndani, nimekuja moja kwa moja kutoka—kutoka Marekani kule, moja kwa moja kutoka Detroit, hapo Windsor, lile jumba kubwa la mikutano.

²⁰⁵ Basi mtu huyu akapanda kuja pale amevalia suti ya kijivu, tai nyekundu, mtu anayeonekana mwenye akili,

nadhifu kwelikweli. Akaja jukwaani. Nami... akasogea. Nami nikasema, “Vema, hebu nipe mkono wako.” Nikasema, “Nimechoka; nimeona maono mengi sana. Hebu tu nipe mkono wako.” Na—nami sikumwangua mtu huyo. Naye akauweka mkono wake juu ya wangu. Ndipo nikasema, “Bwana, huna kasoro. Nenda zako.”

Yeye akasema, “Loo, ipo, pia.”

²⁰⁶ Ndipo kasema, “Vema, hebu niangalie pale.” Nikasema, “La, bwana, hapana hata ishara moja. La, bwana, wewe ni mtu mwenye afya.”

Akasema, “Nenda kaangalie kadi yangu ya maombi!”

²⁰⁷ Nikasema, “Sijali ulichoandika kwenye kadi yako ya maombi.” Nikasema, “Mimi sina uhusiano wo wote na kadi ya maombi,” bila kufikiria, mnaona. Nilikuwa nimechoka na kudhoofika. Na nini hii yangu... Lakini neema ya Mungu, mnaona, ilikuwa ingali pale, kumbuka.

²⁰⁸ Kama akikutuma, ni wajibu Wake kukulinda. Si wangu; ni Yeye. Yeye alilituma. Mimi ninapaswa tu kusimama kwenye lile lililo Kweli.

²⁰⁹ Musa alipoitupa fimbo yake chini, iligeuka ikawa nyoka, nao wale wachawi wakafanya jambo lile lile, Musa angalifanya nini ila kusimama pale na kungojea neema ya Mungu? Hivyo tu. Jambo lile lile. Yeye alifuata amri. Nanyi mnajua nini kilitukia, siyo? Mnaona?

²¹⁰ Mtu huyu alisema, “Naam,” yeye alisema, “ipo. Angalia kadi yangu ya maombi.”

²¹¹ Nikasema, “Vema, heunda ulikuwa na imani nyingi sana, na huenda ilikuponya,” bila ya kufikiria, mnaona. Nilifanya... bila hata kuangalia.

²¹² Ndipo anafungua koti lake na kutoa mbele kifua chake. Akasema, “Haya basi!” akielekea ule mkutano.

Nikafikiri, “Nini kinaendelea hap?”

²¹³ Akageuka. Akasema, “Haya basi!” Kasema, “Mnaona hicho kiinimacho?” Huyu hapo Yuda wako, mtu wa dini, mhubiri wa madhehebu makubwa. Kasema, “Haya basi! Ati nilikuwa na ‘imani nyingi sana.’ Sasa, amekuwa mdhaifu sana, hawezi kusoma uweza wa kushirikishana mawazo. Mnaona, haumjii tena.” Naye pale akasema, “Si kwamba imani yangu ilikuwa nyingi sana.” Kasema, “Niliandika hayo kwenye kadi ya maombi, na sasa yeye hawezi kulijua, mnaona.” Kasema, “Hicho ndicho kiinimacho!”

²¹⁴ Nikawaza, “Kuna nini?” Ndipo neema ya Mungu ikashuka.

²¹⁵ Nikasema, “Bwana, mbona ibilisi ameweka moyoni mwako kujaribu kumdanganya Mungu?” Yuda wa kisasa! Nikasema, “Wewe ni mfuasi wa kanisa la Kristo...” Samahani. Vema,

tayari nimelitaja. “Wewe ni mhubiri wa kanisa la Kristo. Wewe u wa kanisa la Kristo, kutoka Marekani. Na mtu huyo anayeketi pale na suti ile ya kijani kibichi, na mke wako na mke wake wanaoketi pale, ninyi mliketi mezani jana usiku iliyokuwa na kitu cha kijani kibichi juu yake, ki— kimetandazwa namna *hii*, nanyi mkaamua kwamba hii ilikuwa ni ‘uwezo wa kushirikishana mawazo,’ nanyi mlikuwa mkija usiku wa leo.”

²¹⁶ Mtu yule akainuka. Akasema, “Hiyo ni kweli kabisa. Mungu, nirehemu!”

²¹⁷ Nikasema, “Bwana, uliweka ‘TB na kansa’ kwenye kadi hiyo, na sasa unayo. Ni yako sasa.”

Ndipo akanishika kwenye mguu wa suruali ndefu, akasema, “Mimi siku- . . .”

²¹⁸ Nikasema, “Siwezi kukusaidia. Nenda zako mara moja. Hilo ni juu yako wewe na Mungu. Uliandika maangamizi yako moja kwa moja kwenye kadi yako.” Basi hayo yakampata. Hivyo tu.

²¹⁹ Mnaona, waamini wa kujifanya, wadanganyifu, wakijaribu kupata kosa kwa Mungu na kwa Neno Lake. Hao ndio akina Yuda. Ndio hao. Mnaona jinsi Yuda alivyotoka? Mnaona jinsi jamaa huyo anavyotoka? Hivyo ndivyo waamini wa kujifanya walivyo. Mnaona, waamini wa kujifanya, loo, wenye elimu sana, wakati mwingine, na shindano kubwa la kuamua linakuja kati ya Neno na kanuni yao ya imani. Na, linapofanya hivyo, wao wanajiua kwa madhehebu yao kama mtangulizi wao, Yuda, alivyofanya hasa. Yuda alijiua kwa madhehebu yake; akamuua Yesu, Neno, kwa madhehebu yake, kisha akamsaliti Yesu Kristo baada ya kudai kuwa yeye ni sehemu yake.

²²⁰ Wahudumu wakati mwingine wakidai kwamba wao ni sehemu ya Kristo, na wakati Neno limetambulishwa kwelikweli kuthibitishwa kwa ajili ya siku hiyo, ya kwamba ni Ujumbe wa wakati huu, nao watajiua kule wapate kupendwa na watu, kwa madhehebu yao; sawasawa kabisa na alivyofanya Yuda, kumsaliti Yesu kwa Mafarisayo na Masadukayo. Roho hiyo haifi, kwa hiyo hapo ni miongoni mwa waamini, waamini wa kujifanya, na wasioamini. Mnaona, hilo ni kweli kabisa, akashuka moja kwa moja akaja akamuua Yesu kwa vipande thelathini vya fedha; na watu wengi watafanya jambo hilo leo kwa ajili ya riziki, kwa ajili ya dolla mia zaidi kwa juma; kweli, wanamkana Mungu anayesimama katikati yao, aliyeyaleta Maisha yao, na pamoja na Neno kamili.

²²¹ Nao watasema, “Loo, siku hizo za miujiza zimepita! Ama, Mungu hahitaji kitu kama hicho leo.” Mnaona? “Loo, ninaamini katika Yesu Kristo, Mwana wa Mungu! ‘Salamu Maria, mama ya Mungu, umebarikiwa kati ya wanawake!’” Mambo haya mengine yote wanayosema! Na baadhi yao walisema, “Ninaamini katika Imani ya Mitume. Ninaamini katika Mungu

Baba, Mwenyezi, Muumba wa mbingu na nchi. Ninaamini katika kanisa Katoliki la Kirumi, na mambo haya yote.”

²²² Niambiini ni lini mtume ye yote alipowahi kuwa na imani kama hiyo. Kama mitume walikuwa na kanuni moja ya imani, imeandikwa katika Matendo 2:38, “Tubuni mkabatizwe, kila mmoja wenu, katika Jina Lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.” Kama kuna kanuni yo yote ya imani kwao, ilikuwa ndiyo hiyo. Wao hawakuwa na kanuni ya imani. Ilikuwa ni Neno. Hiyo ni kweli. Lingali linadumu vile vile. Hayo ndiyo maagizo ya daktari kwa tiba ya ugonjwa wa dhambi, “Nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu! Tubuni mkabatizwe mpate ondoleo la dhambi, mnaona, naye mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.”

²²³ Bali wao wanajiiza, kama vile Yuda. Huyu ndiye yule mwamini wa kujifanya. Wengine wao ni watu wenye akili nyingi sana. Basi huyu mwamini wa kujifanya, mwangalie jamaa huyo. Huyu ndiye yule jamaa mwerevu. Jamaa huyo mdogo anayejaa upesi, na kuruka juu na kukimbia zake nje, kwa kila tamshi dogo ambalo halimpendezi, usimjali; yeye ni asiyeamini, kwanza. Bali unapomwona jamaa huyu, mwamini wa kujifanya, anasitasita, mnaona, huyo ndiye Yuda. Huyu ndiye.

²²⁴ Kama vipawa vikuu. Nitataja majina hapa. Ambalo, kweli hainipasi kufanya jambo hilo, bali nitayataja, hata hivyo, ili kwamba mpate kujua jambo hilo. Kama vile, Elvis Presley, Red Foley, Ernie Ford, Pat Boone. Elvis Presley, Mpentekoste; Pat Boone, kanisa la Kristo; Red Foley, shemasi katika kanisa la Kristo; nami nafikiri Ernest Ford ni Mmethodisti. Na watu wote hao walio na vipawa, werevu, kwenye matelevisheni. Huku watu wakisema, “Vema, si hao ni wa dini? Wanaimba nyimbo.” Hilo halimaanishi hata kitu. Naam, bwana. Wakiudanganya ulimwengu!

²²⁵ Wao wanapata nini kwenye jambo hilo? Yuda alipata vipande thelathini vya fedha. Elvis, mlolongo wa Makadilaki, na dolla mia moja, ama mbili, dolla milioni mia moja na hamsini ama dolla milioni kwa santuri na vitu kama hivyo. Pat Boone na hao wengine. Sijali hao ni wafuasi wa kanisa gani, na kila kitu, ni unfiki. Ni viinimacho. Ni ufidhuli. Hayo, maisha yao yanathibitisha wazi, hilo si sawa. Basi.

²²⁶ Halafu kuna wale walio na vipawa ambao ni viongozi wakuu, hekima ya kilimwengu. Wanahubiri Injili, wanadai wanahubiri; watu werevu, wenye akili nyingi. Sikilizeni, mtu aliyefunzwa katika fani hiyo, yeye si mhubiri. Yeye ni mtoa hotuba. Hapo ndipo penye shida leo, tuna watoa hotuba.

²²⁷ Yesu hakusema kamwe, “Enendeni mkawafundishe kufanya jambo hili.” Alisema, “Enendeni mkaihubiri Injili, na ishara hizi zitafuatana na mahubiri.” Mnaona? Mnaona?

228 Hiyo si kujifunza kumfanya mtoa hotuba anayeweza kusimama na kunini hii tu, jamani, kuweka vitu vyenye umaridadi mle, ambavyo vinakufanya ujisikie umeketi moja kwa moja mbele ya Malaika Mkuu. Si hilo. “Wenye mfano wa utauwa,” mnaona, huyo ni mtoa hotuba, si Roho Mtakatifu katika matendo.

229 Maskini jamaa mdogo ambaye asingejua ABC zake, huenda akashuka na Nguvu za imani pamoja na Neno; na kumfanya Roho Mtakatifu atende mambo ambayo mtu huyo hajui kitu juu yake, na kulikana. Mnaona? Haya basi.

230 Watu mashuhuri! Naam, bwana. Halafu, wao ni viongozi. Wametajirika, wamefanikiwa, ni werevu katika hekima ya kilimwengu.

231 Kama tu vile kabisa Shetani alifanya kwa Hawa, maskini mwanamke huyo mdhaifu. Yeye alikuja moja kwa moja kwake na kujaribu kumuuzia wazo kwamba angekuwa na hekima kuliko alivyokuwa, na jambo hilo ndilo alilokuwa anatazamia. Badala ya kukaa moja kwa moja na yale Neno lilisema, yeye—yeye alitaka kumuuzia wazo kwamba angekuwa na hekima zaidi, naye akanunua bidhaa yake. Nao wangali wanafanya jambo lile lile leo. “Hekima ya dunia hii ni upumbavu kwa Mungu.” Naam, bwana.

232 La, bwana! Loo, jamani, kitu kile kile tu walichokuza Mafarisayo, nao wakafanya, mnaona, kwa hekima waliyojua. Lakini, lakini wao wanakana Neno lote la Mungu.

233 Wakati limehakikishwa kikamilifu na limethibitishwa kwao, wao wangali wanajaribu kutafuta kitu fulani, na kufikiri ni kiinimacho. Wao hawajatosheka mawazoni mwao. Hawawezi kuliadini. Unaweza kuwaambia cho chote, nao wamerudi tena; unaweza kuwaambia lo lote, nao wamerudi tena. Nao wanadini hii tu. . . Wala hawawezi kulifanya likolee ndani, mnaona. Hebu waangalie; wao wanangojea wakati, mwanya tu. Hivyo tu ndivyo wanavyotaka.

234 Hivyo ndivyo, isingalikuwa ni kwa ajili ya neema ya Mungu, mianya yangu yote ingewekwa wazi, kama ningalikuwa na yo yote. Mnaona? Ni neema ya Mungu, maana hakuna mianya katika Neno la Mungu; ni Injili dhahiri tu. Daima nimesema, mtu ye yote, kama ukiniona nikifanya ama nikifanya jambo lo lote ambalo haliambatani kabisa na Neno la Mungu, wewe njoo uniambie. Hiki hapa kitu kinachofunika mianya ambayo unajaribu kupata. Likazie macho tu Hilo, nawe hutaona mianya, yo yote, maana hakuna mianya.

235 Sasa kumbukeni, Yuda alifikiri ameona mmoja. Jamaa huyo alifikiri ameona mmoja. Mara nyingi, wanafikiri wanauona, bali inathibitika kwamba si mwanya. Hao ndio waamini wa kujifanya, wanafiki. Wao wako asilimia tisini na tano kwenye Neno, ndivyo alivyokuwa Hawa, lakini, tisini na tisa na tisa kwa

kumi; lakini hiyo moja juu ya kumi ndiyo iliyosababisha mauti yote na huzuni.

²³⁶ Hilo ndilo jambo moja linaloyahukumu madhehebu na kadhalika, maana wao hawalichukui Neno lote la Mungu. Hao ni waamini wa kujifanya. Tunaona ya kwamba imekuwa hivyo daima, bali wao wanakana Neno la kweli, lililothibitishwa. Hawa daima wako katika kila kizazi. Tunawaona wanapoendelea tu, na pia wa dini sana.

²³⁷ Naam, ninakaribia kufunga sasa hivi, maana tayari nimechukua nusu saa nyingine.

²³⁸ Yesu, tunaona ya kwamba ametuonya dhidi ya siku hizi za mwisho na watu wa aina hii, ya kwamba wao watafanana sana na kitu kilicho halisi, hata wangewapoteza kabisa walio Wateule. Ni kitu gani hicho? Hao ni akina Yuda, watu ambao wanaenda juu kiasi *fulani* tu. Angalieni, wao—wao hata wanaweza kulia, kupaza sauti, kudai wanaweza kutoa pepo, kila kitu, kisha wageuke na kulikana Neno. Kabisa. Wao wana mfano wa utauwa. Wao—wao—wao karibu wange- . . .

²³⁹ Angalia mahali Yuda alipofikia. Roho ya Yuda ilipanda katika Injili, ikafikia mpaka kwenye Pentekoste. Bali ilipofikia mahali pa kubatizwa kwake katika Jina la Yesu Kristo, na mambo haya mengine yanayoambatana na ubatizo wa Roho Mtakatifu, alitoka akaenda zake. Alionyesha rangi zake. Basi roho hiyo inaweza kuishi katika madhehebu hayo mpaka inapofikia moja kwa moja kwenye Kweli, ndipo inashuka kurudi moja kwa moja, kama roho aliye juu yao, aliyewatangulia kuja kwao; kama tu vile Yohana alivyokutangulia kuja kwa Yesu.

“Sasa unasema, ‘Yesu alisema wangepanana sana.’”

²⁴⁰ Naam, “Waloteuliwa,” hao ndio aina ile ambayo wameandikwa majina yao kwenye kile Kitabu, tangu kuwekwa misingi, ya Uzima, ambao wanaamini, ama misingi ya dunia, ambao wanaamini Neno lote la Uzima. Hao ndio wale walioteuliwa.

²⁴¹ Sasa waangalie watu hawa. Naam, ninasema jambo hili kwa kicho na heshima, pamoja na upendo wa kiungu; kama mimi sifanyi hivyo, mi—mi—mi—mimi ninahitaji wito wa madhabahuni, mimi mwenyewe. Angalia, Yesu alisema wangewapoteza walio Wateule. Naam, hao wasingekuwa Methodist, hao wasingekuwa Baptisti; tunajua wao ni wasioamini, kwanza. Lakini, ni mashirika ya Kipentekoste yaliyounda madhehebu hayo, wakachora mistari yao, bila ya Neno; wakachora mstari na kuweka madhehebu yao wenyewe, wakalifungia Neno nje. Wangewapoteza Walioteuliwa, wanafanana sana sana! Husema, “Wanalia. Wanapaza sauti. Wanaruka-ruka. Wanadai ibada za kuponya.” Ndivyo alivyofanya Yuda, na ndivyo walivyofanya wengine wao.

Walipotoka, wakarudi wakifurahi na kila kitu, na hata majina yao yaliandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo.

²⁴² Lakini, kumbukeni, Bibi-Arusi ha—ha—hapatikani kwenye kundi hilo. Yeye anapaa juu katika Kunyakuliwa.

²⁴³ Kwenye ile Hukumu, hukumu iliwekwa, “Na vitabu vilifunguliwa, wale waovu; na Kitabu kingine, ambacho ni Kitabu cha Uzima, kilifunguliwa,” naye Bibi-arusi alikuwa pale apate kulihukumu. Mnaona? Mnaona? “Kitabu kingine kilifunguliwa, ambacho ni Kitabu cha Uzima.” Hao ni kondoo walio upande mmoja, na mbuzi upande mwingine. Mnaona, watu waliokufa huko nyuma, wasiokuwa na nafasi, hao ndio watakaobaguliwa.

²⁴⁴ Lakini sasa angalia, “kuwapoteza” Walioteuliwa, liangalie kundi hilo. Hilo ndilo kundi lile linalofuata moja kwa moja, “Naam, ndugu. Haleluya! Naam. Utukufu kwa Mungu!” Na kule ndani kabisa moyoni mwako unaona kile wanachokufanyia; wanakualika kanisani (kwa nini?) kuuvutia umati wa watu, kuwakamua kila kipande cha fedha wanachoweza kupata kwenye jambo hilo. Mnafikiri mimi sijui jambo hilo? Huenda wasifikiri mimi ninajua jambo hilo, bali ninalijua.

²⁴⁵ Yesu alijua, tangu mwanzo, ni nami aliyekuwa mwongo. Unaona? Unaona? Lakini alifanya nini? Yeye alingoja tu hadi wakati huo. Hilo ndilo linalotupasa kufanya daima, kungojea mpaka wakati huo. Usiingie mwenyewe. Ngojea mpaka dakika hiyo.

²⁴⁶ Wakiwa na pi-...mfano, nao wanaendelea moja kwa moja, hilo ndilo kundi lile linalodanganya. Mwangalie huyo mdanganyifu, kundi hilo pale; si—si mwamini, si asiyeamini, bali huyo mwamini wa kujifanya. Loo, jamani! Wao wanafanya kitu gani? Wananyemelea tu mpaka watakapofikiri wanaweza kupata kitu fulani, wakichomoa kila peni wawezayo kuchomoa kutoka kwa watu, mnaona, kisha wanazilundika kwenye madhehebu haya makubwa mno; ambayo yanapinga kabisa, nao wanajua jambo hilo. Mnaona, wanajua.

²⁴⁷ Unalosema halileti tofauti yo yote. Wao daima wamekwisha kuwaonya watu wao kabla hujaja, “Msisikilize jambo Hilo.”

²⁴⁸ Mtu mmoja, mwenye ujasiri wa kusimama kule Ohio, mara tu Ndugu Kidd alipoponywa, alikuja pale jukwaani, na kusema, “Naam, Ndugu Branham ni nabii, hapana shaka kabisa, wakati yuko chini ya upako. Lakini sasa,” kasema, “wakati ule upako umemwacha,” kasema, “msiamini Mafundisho yake, kwa maana si sahihi.”

²⁴⁹ Naye hakujua, ya kwamba nilipokuwa nimeketi chumbani mwangu, Bwana alinifunulia jambo hilo. Nami nikaenda mara moja pale. Na wengi wenu mlikuwa kule. Nikasema, “Kwa nini mtu angesema jambo kama hilo, wakati Neno...” Naam, mnaona, mimi sikusema kwamba nilikuwa nabii; yeye alilisema.

²⁵⁰ Basi nabii, neno *nabii*, “mwonaji,” Agano la Ka- . . . Naam, tafsiri ya Kiingereza ya *nabii* humaanisha “mhubiri.” Lakini *mwonaji* wa Agano la Kale alikuwa ni mtu aliyekuwa na “mafafanuzi ya Kiungu ya Neno,” naye alithibitishwa na Neno likija kwake na kuliona hapo kabla. Hivyo ndivyo ilivyokuwa . . .

²⁵¹ Basi mtu kusema kwamba mtu ni nabii, kisha kusema kwamba Mafundisho yake si sahihi? Kama hiyo si njama ya kupata pesa, ni kitu gani? Saa imekaribia wakati kitu hicho kitabururwa kiwekwe hadharani. Naam. Lakini hao ndio aina ambayo, huyo mwamini wa kujifanya, anayekupigapiga mgongoni, anakuita “ndugu,” kama tu Yuda. Lakini, kumbukeni, Yeye alijua tangu mwanzo. Yungali anajua. Naam, bwana.

²⁵² Kumbukeni, wote hawa mnaosikiliza kanda hii, pia, hiyo ni kweli, ninyi mmo katika moja ya tabaka hizo. Hilo ni kweli kabisa. Sasa tutafunga. Kila mtu aliyepo hapa, aliyeko, kila mtu anayesikiliza kanda hii; na hata ingawa siku moja sina budi kuondoka humu duniani, kanda hizi zingali zitaendelea. Hiyo ni kweli. Mnaona? Nanyi mmo katika moja ya tabaka hizi. Huna budi kuwa katika moja ya hizo. Ni kweli kabisa. Hamwezi kuliepuka jambo hilo. Mmo katika moja ya tabaka hizi.

²⁵³ Sasa nini? Jitambulisha mwenyewe na mtu wa Biblia ambaye aliamini, ambapo uliamini Neno wakati lilipothibitishwa, kama nilivyothibitisha jambo Hilo usiku wa leo, kwamba lilikuwa ni Neno lililothibitishwa daima, daima linapingana na imani inayopendwa na watu wengi.

²⁵⁴ Kama ungaliishi katika siku za Nuhu, sasa hebu niulize tu, ungekuwa upande gani, upande wa kanisa ama upande wa Nuhu, yule nabii? Mnaona?

²⁵⁵ Kama ungaliishi katika siku za Musa, ungaliamini ujumbe wa Musa baada ya kuhakikishwa na kuthibitishwa na Mungu? Lakini ungaliambatana na Kora na Dathani, na hao wengine, na kusema, “Wewe siye pekee uliye mtakatifu. Watu wengine wanaweza kufanya mambo haya unayofanya, pia”? Unaona? Ingekubidi uwe mmoja, nawe ndivyo ulivyo, usiku huu.

²⁵⁶ Ama ungalikuwa pamoja na Danieli, ama na kanisa lililokuwa kule chini kwenye karamu ya Nebkadreza waliyokuwa wakisherehekea? Mnaona? Je! ungalikuwa nje, ama ungalikuwa kule chini kwenye makelele, lile—lile jambo kubwa walilokuwa wanasherehekea?

²⁵⁷ Je! ungalikuwa na Eliya, mtu huyo anayesimama peke yake, aliyeitwa, “mzee mwenda wazimu, mtu aliyerukwa na akili,” huku amesimama juu ya kilima, na kichwa chake kinawaka hapo kwenye jua, ameshika fimbo iliyo-pinda mkononi mwake, nao ndege wanamlisha, a-ha, mwenda wazimu fulani? Ama ungalikuwa pamoja na wale makuhani na hao wote kule chini pamoja na Yezebeli, na hao wanawake wengine waliovalia

kisasa? Naye Eliya, akisimama kule juu, anawakemea, kwa nguvu alivyoweza! Ni upande gani ungalimpeleka mke wako? Wazia tu. Jialangie tu usiku wa leo.

²⁵⁸ Katika siku za Yesu, ungalikuwa na mvulana huyu asiye kuwa na kitambulisho? Yeye hakuwa amejiumba na madhehebu yote. Walisema, “Ulitokea shule gani? Wewe humo katika orodha Yetu hapa. Ulipata wapi hekima hii? Ungepataje kujifunza kama hatukukufundisha mambo haya? Ulipitia shule gani? Wewe ni Mmethodisti, Mpresbiteri, ama Mbatisti?” Yeye hakuwa mojawapo wa hayo. Hiyo ni kweli. Yeye alikuwa Neno. Hiyo ni kweli kabisa, ndugu. Hivi wewe. . .

²⁵⁹ Ama ungaliungama na Mafarisayo wa imani ya kisasa ya maskini mzee kasisi mnyenyekevu aliyeonekana mpole sana na mzuri, na madhehebu yale yaliyosimama tangu lile Baraza la Nikea, ama tangu Luther alifanye madhehebu? Ama ni kundi lipi—lipi ungalijiunga nalo? Hivi ungekuwa kwenye. . . Ungalikuwa na kundi lipi? Ungalisimama pamoja na Neno ulipoliona limethibitishwa na kuhakikishwa kwako, lilikuwa Ujumbe wa zamani hizo, ama ungalichukua msimamo wa kanisa? Sasa hebu tu jialangie mwenyewe usiku wa leo.

²⁶⁰ Ungalikuwa pale pamoja na mitume, wakati walipomwona Yesu na mambo haya yote ya ajabu, wakati alipowakemea hao wahubiri, na kusema, “Ninyi ni kiota cha majoka”? Hao wazee wahubiri waaminifu, waliolisoma Neno hilo. Kasema, “Ninyi si kitu ila tundu la wanyanga’anyi, nanyi—nanyi mmejaa mifupa ya wafu. Ninyi si kitu ila kuta zilizopakwa chokaa.” Mnaona? “Enyi kizazi cha majoka.” Ungalisimama na Jamaa mwenye hasira kali namna hiyo, Ambaye alisimama pale na kukemea na kurarua? Kasema, “Ni nani kati yenu anayeweza kunishuhudia Mimi kuwa nina dhambi? Nisipotenda aliyosema Baba Yangu. . .”

²⁶¹ Wao walisema, “Msisikilize. Jamaa huyo ana pepo mchafu ndani Yake. Ana kichaa. Yeye ni wazimu. Yeye ame—amepagawa na ibilisi. Mnaona? Naam, jinsi anavyofanya jambo hilo, Yeye, hiyo ni roho ya mwaguzi ndani Yake. Anawaambia. . . Yeye ni nini? Mama yake alimpata kabla yeye na mumewe hawajafunga ndoa. Mnaona? Mnaona? Yeye alipitia shule gani? Hatuna hata kumbukumbu moja Yake kwamba alipitia katika shule ya sekondari kamwe.”

²⁶² Na hata hivyo Yeye alipokuwa na umri wa miaka kumi na miwili, aliwashangaza na kuwapumbaza makuhani, kwa Neno la Mungu. Mnaona? Yeye alitokea shule gani? Shule ya Huko Juu. Mnaona? “Mtakapomwona Mwana wa Adamu akipaa kutoka alikotoka.” Mnaona, hiyo ilikuwa ndiyo shule Yake.

²⁶³ Lakini ungalisimama na wale mitume, kwa Mtu kama huyo, wakati shindano la kuamua lilipokuja?

²⁶⁴ Ama wewe kweli ungaliondoka pamoja na wale sabini, na kusema, “Vema, tutarudi makanisani mwetu kama hivyo ndivyo

utakavyofundisha, ukisema ya kwamba, ati Wewe, ‘Mwana wa Adamu’”? Basi, hata hivyo, u nani Wewe? Wewe ni kitu gani? Mtu kama nilivyo mimi, ninakula pamoja Nawe, na huku unajaribu kusema ati Wewe ni kitu fulani. Nimekuangalia. Nimeona udhaifu Wako. Nimekuona ukilia. Nimekuona ukifanya *hivi, vile*, ama *vinginevyo*. Nimekuona ukienda jangwani pamoja nasi, na kila kitu namna hiyo sasa, Nawe u mwanadamu tu. Halafu unasema ati ulishuka kutoka Mbinguni. Hilo limenishinda.” Ungalitembea pamoja nao? Ama ungaliondoka pamoja na wale sabini? Ama ungalitembea pamoja na mitume na Kristo?

²⁶⁵ Wakati Mtakatifu Martin alipojaribu kushikilia ubatizo katika Jina la Yesu Kristo, kanisani, wakati alipojaribu kushikilia ishara na maajabu na kadhalika, nalo kanisa Katoliki likamhukumu mtu huyo wala lisingemtambua hata kidogo, na kumtupa nje, je! wewe ungalijiunga na kanuni ya imani ya Katoliki, ama ungalisimama na Mtakatifu Martin? Wakati alipokataa kuweka namna hizi zote za sanamu za—za watu waliokufa, na kuziabudu, kuabudu sanamu hizo, na kadhalika, wakati alipokataa mafundisho ya sharti yaliyoongezwa, akasema, “Neno na liwe Kweli!” Naye Mungu akamthibitisha kwa ishara kuu na maajabu, na yale aliyotabiri yalitukia. Na kila kitu alichofanya, yeye alitembea katika Roho wa Mungu na kuthibitisha jambo hilo, na hakuna hata mmoja wa hao makuhani wala cho chote kile kingefanya lo lote kuhusu jambo hilo. Je! wewe ungalichukua msimamo wake na kuambatana na Mtakatifu Martin, ama ungaliambatana na kanuni ya imani ya Kikatoliki?

²⁶⁶ Sasa Neno, sasa Neno la Mungu ama mafundisho ya sharti ya kanisa, viko mbele yako. Unaweza kuchukua, kukubali kile mafundisho ya sharti ya kanisa, ama utachukua kile lisemacho Neno?

²⁶⁷ Kumbukeni, katika nyakati zote imekuwa kama ilivyo sasa hivi. Daima kuna imani inayopendwa na watu miongoni mwa watu, na daima imekuwa ikipingana kidogo tu na Neno halisi. Kumbukeni, haijakuwa kamwe ni kulikataa kata kata. Loo, la. Mpinga Kristo hakani Neno. La hashu. Yeye anasema analiamini, bali si lote jinsi lilivyoandikwa hapa. Mnaona? Mnaona?

²⁶⁸ Shetani alimwambia Hawa. Hawa aliliamini lote ila kile kipengele kidogo alichomwambia. Wao huchukua tu lote ila kipengele kidogo tu. Huenda ikawa ni, “nenda kwenye kidimbwi,” huenda ikawa ni jambo lingine. Huna budi kulichukua, kila kipengele, jinsi tu lilivyo *Hapa*, mnaona, jinsi tu lilivyonewa *Hapa*. Huenda likakufanya kurudia baadhi ya kazi za kwanza tena, bali ni kile tu Neno lilichosema. Hii imekuwa ndiyo njama ya Shetani tangu alipoitekeleza mara ya kwanza kwa Hawa, kutokuamini sehemu ndogo tu ya Neno.

269 Basi, daima linabagua tabaka hizi tatu za watu, Neno hubagua watu hawa. Katika kila kizazi imekuwa hivyo. Kila kizazi kilichowahi kuweko, imekuwa namna hiyo, ambapo Mungu alituma kitu fulani hadharani na anakithibitisha dhahiri, Neno Lake.

270 Halafu kuna wale wanaofuata, ambao wanadai kuwa waamini, nao ni waamini. Kuna hao ambao wasingerudi nyuma. Wao wanaliamini Neno. Mradi tu unadumu katika Neno, wao wanaliamini.

271 Bali lijapo ni kinyume kidogo, haidhuru Mungu analitambulisha kiasi gani kwa yale wanayoamini, wao wanasema, “Vema, si—si—sijui kuhusu jambo *Hilo*.” Huyu ni asiyeamini.

272 Ama unafuata ili tu kuona mpaka upate nafasi ya kusema, “A-ha, kumbe!” Yuda fulani kumsengenya mtu kisiri, kama alivyofanya. “Nilijua jambo hilo lingekuwa wazi, hakuna budi. Haya basi!” Huyu ni mwamini wa kujifanya. Kila, kila kipengele chake, twaona jambo hilo katika Biblia.

273 Maskini mvulana mmoja wakati mmoja, hapa chini Kentucky, aliyelelewa huko juu kabisa milimani, yeye—yeye hakuwa amewahi kuwa mahali palipokuwa na kioo cha kujiangalia. Alikuwa na kipande kidogo kilichotundikwa juu ya mti, bali hajawahi kujiona mwenyewe. Alikuwa hapa Louisville, ilisimuliwa, akakaa na dada ya mama yake. Naye aliishi katika moja ya nyumba nzuri, nyumba ya mtindo wa kale. Walipoingia katika kimoja cha vyu—vyumba vya kulala vilivyokuwa na m—mlango uliokuwa na kioo juu, chini hadi juu. Mnaona?

274 Basi wakati yule jamaa mdogo alipoanza kukimbia kila mahali mle nyumbani, akasimama. Mtoto Johnny akamwona mtoto Johnny. Mnaona? Ndipo akajikuna kichwa, naye mtoto Johnny kwenye kioo akajikuna kichwa. Akacheka, naye mtoto Johnny kwenye kioo akacheka. Akaruka-ruka, naye mtoto Johnny kwenye kioo akaruka-ruka kwenye kioo. Mnaona? Akasogea karibu sana. Alifikiri ni mvulana mdogo angaliweza kucheza naye, kwa hiyo akasogelea. Mara, akapigapiga kile kioo. Akageuka, na wazazi wake walikuwa wanamwanguka. Akasema, “Mama, yule ni mimi.”

275 Sasa angalia katika jambo *Hili*, basi wewe ni yupi? A-ha. A-ha. Ni yupi *kati* ya *hawa* Johnny wadogo unayemwiga? Wewe ni yupi, unaona? Wewe ni mmoja wa hao.

276 Huyu ni mmoja wa hao, yule ambaye angerudi, kosa la kwanza ulilopata uliloita kosa. Mnaona?

277 Lijaribu kwa Neno uone kama ni kweli, kama Neno huthibitisha mambo yote. Mnaona, thibitisheni mambo yote kwa Neno. Yesu alisema ufanye hivyo. Naam, bwana. “Shikilia yaliyo mema.” Hivyo ndivyo alivyosema hasa.

278 Basi angalia kwenye kioo cha Neno la Mungu, katika nyakati zile nyingine, uone ni kundi gani la haya matatu ambalo ungejitambulisha kwalo. Sasa wazia tu, kama ungaliishi katika siku za Nuhu, kama ungaliishi katika siku za Musa, kama ungaliishi katika siku za Yesu, ama mmoja wao, cho chote kile, wazia tu ni kundi gani ungalitambulishwa nalo. Wazia jambo hilo usiku wa leo.

279 Halafu, hali yako ya sasa. Naam, wazia sasa. Hili lina kilindi sasa. Wala usilikose. Hali yako ya sasa sasa hivi inakuthibitishia ni kundi gani ungalikuwa nalo kule nyuma. Naam, ninyi ni mahakimu wenu wenyewe, inathibitisha ulivyo wewe.

280 Kasisi, mhudumu, ungalikuwa na kundi gani wakati Yesu alipotoa tamshi lile lililokuwa gumu kuamini? Ati nini? Ati nini? Baada ya Yeye kutambulishwa kwelikweli kwamba alikuwa ndiye Neno, mnaona, hata hivyo, tamshi hilo, hujasikia jambo kama hilo, "Mwana wa Adamu, mtasema nini kama Yeye akipaa huko juu Mbinguni Ambako alitoka?"

281 Nanyi mlisema, "Vema, ninajua alikozaliwa. Ninamjua baba Yake, ninamjua mama Yake, naye hapa anasema atapaa kutoka mahali alikotoka." Jambo hilo kidogo lingekushinda, sivyo, bwana? A-ha. Kidogo lingekushinda; usingaliweza kuvumilia Hilo. Labda ni jambo lile lile leo. Basi angalia kwenye kioo cha Neno la Mungu uone unakosimama. Loo, ewe mwenye kuwadanganya watu, usifanye jambo hilo kamwe.

282 Angalia, wewe umo katika moja ya tabaka hizi. Katika hali yako ya sasa hivi, hali yako ya sasa ya akili, kwamba, ninyi mlio hapa katika mkutano huu unaoonekana, nanyi mtakaokuwa katika mikutano isiyoonekana ya kanda hii, hali yako ya sasa ya akili baada ya kuisikiliza kanda hii, inakuthibitishia uko katika tabaka gani. Inakwambia mahali ulipo hasa, iwapo wewe ni mwamini katika Neno na utadumu Nalo, kama ungeondoka uende zako, ama kufunga kanda hiyo. Unaona, hiyo inaonyesha, kile ulichofanya. Hutaki kuisikiliza, nawe unaifunga, wasema, "Sitaki kusikiliza jambo Hilo," huyo, huyo ni yule asiyeamini. Mnaona, usingesimama na kulijaribu uone kama ni Kweli ama si Kweli. Mnaona? Ama unasitasita tu na kujaribu kupata kosa fulani kwenye jambo Hilo, ndipo unajua mahali ulipo, pia. Inakwambia.

283 Mungu na atusaidie kuamini jambo Hilo na kulitetea, na kuwa waaminifu Kwake, na kulitii Neno, kwa kuwa Yeye ni Neno. Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

Na, na tuombe.

284 Baba Mpendwa wa Mbinguni, jinsi ilivyo vigumu, wakati mwingine, kusema mambo haya, na kujua ya kwamba labda makumi elfu ya watu watayasikia haya kwenye kanda hii, ziendapo kila mahali nchini na kila mahali ulimwenguni. Lakini,

Bwana Mpendwa, ni kweli, ni kweli kabisa. Ninaomba, Bwana, kwanza uusafishe moyo wangu. Ee Bwana, nijaribu mimi, nijaribu.

285 Niangalie tu hapa chini, Bwana. Mimi ni mdhaifu. Ni—ni—ni. . . Ni—nimechoka. Ni—ni mdhaifu. Koo langu limepwelea. Midomo ya—ya—yangu ime—ime—ime—imekauka, yaonekana. Pia, pia mwili wangu unazeeka, ninazeeka. Na—na haitakuwa muda mwingine mwingi sana, Bwana, labda, machweo mengine mengi ya jua, m—m—mpaka nitakuwa ninaondoka.

286 Basi sasa nichunguze, sasa, Baba. Na iwapo—iwapo kuna jambo ninalokosea, nami sijui, Wewe—Wewe nifunulie tu, Bwana. Wewe, Wewe nionyeshe. Niko tayari sasa kulisahihisha lote.

287 Ninajiangalia mwenyewe kule kwenye kioo cha Neno la Mungu. Ninasimama wapi? Hivi ninaona sura yangu ikirudisha mng'ao wa Yesu Kristo? Huyu ndiye mtu ninayemwona kwenye kioo? Ninamwona mmoja wa waamini wa Agano la Kale, ama waamini wa Agano Jipya? Ninaona mwamini wa kujifanya? Ninajiona mwenyewe kama mtu asiyeamini ambaye asingetulia na kusikiliza Neno, na angechukua wazo la kimadhehebu badala yake? Je! ninajiona nikisitasita, nikijaribu kupata mwanya mdogo?

288 Bwana, kama ndivyo ilivyo, ni—nisafishe tu, Bwana. Naomba moyo wangu uwe msafi na mtakatifu. Kwa sababu, haya ni maisha yangu, Bwana, mimi. . . Ni, ninataka yawe sahihi. Hakuna haja ya kulifanya jambo hilo nusu-nusu, iwapo kuna njia ya kulifanya lifanyike kabisa. Mimi, ninataka yatengenezwe vizuri, Baba. Si hilo tu, bali ningekuwa nikiwaongoza wanaume vibaya, na wanawake vibaya, na watu niwapendao, nao wananipenda; basi, ningekosea.

289 Basi, Baba, kama kuna jambo lo lote, kama nilifikiri usiku wa leo kwamba kanisa lo lote la kimadhehebu lilikuwa sawa; ama Baraza la Mekanisa lilikuwa sawa, kama wingi wa watu ulikuwa sawa; Bwana Mungu, nisaidie kuwa mwanamume vya kutosha, na Mkristo vya kutosha, kosa langu nimekosea na kusimama hapa na kuwapeleka watu hawa mahali ninapofikiri kwamba pangukuwa sawa. Nisafishe. Nijalie kuangalia na kuona. Bali inapofikia mambo hayo, Bwana, kadiri nionavyo mimi, wakiwa na taratibu hizo na kulikana Neno; unaweza ukawaambia jambo Hilo, na hata hivyo wao watasema, “Vema, haileti tofauti yo yote. Ni. . . Mungu hatarajii jambo Hilo sasa.”

290 Bwana, ninaamini ya kwamba Wewe ni Yesu yeye yule. Wewe ni Mungu Yeye yule uliyekuwa daima. Wewe ungali ni Mungu, nawe hubadiliki. Ninaamini ya kwamba Biblia hii ni Neno Lako, nami ninaamini ya kwamba Wewe na Neno Lako ni kitu kile kile.

²⁹¹ Pia naomba, Mungu, ya kwamba utatupa Roho Wako Mtakatifu, kulihuisha Neno, kutupa Nguvu ya kuhuisha; ili kwamba, siku moja wakati maisha yatakapokwisha, nawe umemaliza nasi, kwamba tutahuishwa na kupaa juu Mbinguni ambako tulikuwa, katika mawazo ya Mungu, kabla ya kuwekwa misingi ya dunia. Mungu, tujalie.

²⁹² Tusamehe dhambi zetu, Baba. Kama kuna mwanamume ama mwanamke hapa, ambaye anasimama katika ile tabaka nyingine, mbali na waamini wa kweli katika Neno, Mungu, isafishe mioyo yao. Kama kuna ye yote anayesikiliza kanda, ama atakayesikiliza, ninaomba mioyo yao itakaswe, ya kwamba Wewe utawatakaswa, Bwana. Si—sitaki kuwaona wamepotea. Mungu, ninaomba ya kwamba Wewe—Wewe utatusaidia kufahamu ya kwamba kosa moja hali— halitasahihisha lingine. Kuna njia moja tu ya kufanya jambo hilo, hiyo ni kuyaondolea mbali makosa yote mawili, na kujiweka sawa. Pia naomba, Baba, ya kwamba utatujalia jambo Hilo sisi, katika Yesu Kristo Bwana wetu.

²⁹³ Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, mioyo yetu imeinamishwa, sasa nawatakeni mtulie kwa dakika chache tu.

²⁹⁴ Nilipoliona lile ono la jehanamu, kama—kama mvulana mdogo, kutisha kwake. Basi, naweza nikasosea katika jambo hili. Hiyo huenda ikawa ni hofu tu ya yatakayotukia. Huenda ikawa. Sijui. Ilionekana nilikuwa mahali fulani. Lilikuwa ni jambo halisi sana.

Halafu, si muda mrefu uliopita, nilipoiona milki ya waliobarikiwa.

²⁹⁵ Nilipokuwa katika milki ya waliopotea, nililia kwa sauti kuu, “Ee Mungu, usimruhusu kamwe mtu ye yote kuja hapa!” Huwezi, hakuna lugha inayoweza kukusimulia kutisha kwake kulivyo. Hakuna njia kwangu ya kuwaambia. Kama mnaamini kwamba kuna jehanamu inayowaka moto, imejaa moto na kiberiti, hiyo ingekuwa ma—malisho baridi ya kijani kibichi yenye kivuli ukilinganisha na jinsi kutisha kwa hali hii ya kupotea kulivyokuwa, na taabu zinazo—zinazohusu mahali pale.

²⁹⁶ Nami kama nikijaribu kuwazungumzia juu ya mambo ambayo yangepita ufahamu wa mwanadamu, ningali nisingeweza kuwelezea habari za mahali pa waliobarikiwa, jinsi palivyo na amani! Hapana kufa, hapana kuzeeka, hapana kuugua; ni ujana wa daima, afya ya daima, na hapana kufa; Uzima wa Milele, katika ujana waliobarikiwa, wala hamna dhambi wala cho chote kile! Loo, hakuna tu njia ya kulielele- . . . kueleza, kulielezea.

²⁹⁷ Hata yule Mtakatifu Paulo, yeye alisema, “Macho hayajaona, sikio halijasikia, wala halijaingia kwenye mioyo ya

mwanadamu,” huwezi hata kulielewa; hakuna njia ya kulielezea, “yale aliyowawekea Mungu, akiba, wale wampendao.”

298 Basi sasa, kwa kuwa jambo hili hakika ni kweli, hapa na kwenye mkutano usioonekana, tumeonyesha hapa, usiku wa leo, katika moja ya tabaka hizi. Aidha sisi ni waamini halisi . . . Lijaribu kwa Neno. Kama Neno lilisema jambo fulani, nalo kanisa likasema jambo jingine, ungechukua lipi? Angalia kwenye kioo cha Neno la Mungu uone unasimama kwenye tabaka gani. Na kama sivyo ulivyo, usiku wa leo, hapa na kwenye mkutano usioonekana pia, kama sivyo ulivyo, kama huko pamoja na kundi hilo linaloamini, je! naweza kuomba ombi dogo tu kwa ajili yako sasa, ili kwamba uingie katika kundi hilo la wanaoamini?

299 Je! ungeweza kuonyesha jambo lilo hilo, kwa Mungu; huku kichwa chako kimeinamishwa, moyo wako umeinamishwa, macho yako yamefungwa, na mbele za Mungu? Wakati mwingine watu wanaogopa kidogo, mwajua, kwa namna fulani kuinua mikono yao juu, wanamwogopa jirani yao. . . Jambo ambalo, hawapaswi kuwa namna hiyo, lakini wao—wao wanapaswa kukaa, na kusema, “Mimi, mimi nimekosea. Nimekosea.”

300 “Yeye ambaye—yeye anayefunika dhambi zake hatafanikiwa, bali yeye atakayezitubu dhambi zake atapata rehema.” Mnaona? Dhambi ni *nini*? “Kutokuamini,” kutokuamini (*nini*?) Neno.

301 Naam, kama wewe huko katika tabaka hiyo, na kuna mambo ambayo—ambayo unayaona katika Biblia ambayo kwa urahisi tu wewe . . . katika—katika *nini*-hii yako . . . katika—katika akili za—zako, hu—huwezi kuona jambo hilo. Wewe una *nini*-hii tu . . . Unajua Biblia ilisema jambo hilo, lakini una *nini*-hii tu . . . Huwezi kulifahamu, na hata hivyo unataka kulifahamu. Wewe sema, “Mungu, nipe kufahamu. Nitakutii.”

302 Tafadhali inua mkono wako, na useme, “Nikumbuke tunapoomba”? Mungu akubariki. Mungu akubariki. Hilo ni zuri. Mnaona?

303 Kweli fikiria tu jambo hilo, “Kuna kitu fulani katika Biblia ambacho na—na *nini*-hii tu—mimi sikijui kweli? Na—na—nina—ninasikitika nitajikuta katika moja ya hivyo vikundi vingine. Labda nitajikuta na wale sabini, kwamba mimi . . . Kuna mambo fulani tu ambayo mimi . . . Ni vigumu sana mimi kufahamu jinsi ambavyo—ambavyo Mungu angefanya mambo haya, jinsi angekuwa, jinsi Yesu angeweza kuwa yeye yule, jinsi—jinsi mambo haya. Si—sielewi jambo Hilo. Ninataka kulielewa. Ni—ninataka kuliamini. Basi, Mungu, saidia kutokuamini kwangu. Ni—ninataka kuwa sehemu Yake. Ninataka kuwa mshiriki wa Neno. Ninalitaka ndani yangu.”

304 “Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu likae ndani yenu, basi ombeni mtakalo.” Yohana Mtakatifu 15. Tunajua jambo hilo ni kweli. Angalia, “Mkikaa,” si kuingia na kutoka, kuingia na kutoka, lakini, “mkikaa ndani Yangu,” Naye ni Neno, “Nalo linakaa ndani yenu, basi ombeni tu mtakalo nanyi matapewa. Yatakuwa yenu.”

305 “Yeye ayapokeaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, tayari amepita kutoka mautini akaingia Uzimani.” Lakini unaweza kulipokea Neno, kwanza? Unaweza kulipokea Neno, Neno lote, Kristo wote? Kristo ni Neno lililotiwa mafuta. Yeye ni Neno, lililotiwa mafuta.

306 *Kristo* maana yake ni “Mtiwa mafuta,” Neno lililotiwa mafuta kwa ajili ya siku hiyo, lililodhihirishwa, Mwokozi, Mkombozi. Hiyo ni wakati alipokuwa aje, naye alikuwa Mtu huyo mtiwa mafuta atakayepachukua mahali hapo.

[Ndugu Branham anagongagonga mimbara mara kadha.]

307 Sasa ni Roho Mtakatifu katika siku za mwisho, kuangaza Nuru za jioni, akirudisha Imani ambayo imekanyagwa chini, katika madhehebu; akiyahukumu madhehebu na kurudi kwenye ile Imani ya asili, pamoja na Imani ya asili ya Biblia; Biblia ya asili, kuamini kila Neno Lake, si kuliongeza wala kulifanya liseme *hivi* na liseme *vile*. Liseme tu jinsi linavyosema, nawe unataka kuliadini namna hiyo.

308 Kuna mmoja ambaye hakuinua mikono yao, wangetaka kuinua mikono yao, na kusema, “Mungu, nikumbuke?”

309 Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, mama mdogo. Mungu akubariki, wewe, wewe. Sawa. Mungu akubariki kijana mdogo. Mungu akubariki, dada yangu. “Ninamtaka.” Na Mungu akubariki, dada, upande wangu wa kulia. Na akubariki, huko nyuma. “Nataka...” Na Mungu akubariki, kijana mwanamume. Nawe, dada, upande huu. Wewe, ndugu, upande huu mwingine, Bwana akubariki. Mungu akubariki upande wa nyuma. “Nikumbuke tu, Bwana.”

310 Sasa kumbukeni, hamniinulii mikono mimi; mnaiinua kwake Yeye. Moja kwa moja huko nyuma yangu, naam, Bwana anaona mkono wako. Hata kama nisipouona, Yeye anaona. Anajua moyo wako. Anajua kinachopigapiga mle. Anajua nia yako. Anajua kusudi lako ni nini kwenye nia hiyo. Mungu akubariki, ndugu.

311 Mtu mwingine, “Ninataka kuamini Neo lote.” Mungu akubariki. Sawa. Mungu akubariki. “Nisaidie, Bwana, nisaidie.” Bwana anaona mikono yenu. Naam, bwana. Haya basi. “Kuna mambo ambayo si—siwezi kuelewa. Si—sitaki kuwa asiyeamini. Ingawa siyaelewi, nataka kuliadini, hata hivyo. Niko tayari kusema, ‘Bwana Mungu, mimi hapa. Ninataka kuamini. Saidia kutokuamini kwangu, Bwana.’” Mungu awe pamoja nanyi.

Mungu awabariki. Mikono mingi, mingi sana imeinuliwa, ingali inainuliwa.

³¹² Unasema, “Ndugu Branham, jambo hilo linasidia?” Inua mkono wako wakati mmoja, ukiwa na ku—kusudi halisi na la kweli, ndipo uone unavyojisikia juu ya jambo hilo.

³¹³ Umeshuhudia kwamba kuna kitu fulani kidogo maishani mwako, wajua. Kuna kitu fulani kidogo, hutaki kiwe humo, lakini kimo mle, hata hivyo. Unashangaa jinsi jambo hilo lingeweza kutendwa vipi. “Basi, Bwana, zuia kwamba nisiwe Yuda. Zuia kwamba ningefuata U—Ujumbe, labda tu nikijaribu kufikiri ya kwamba siku moja kosa dogo litazuka. Ee Mungu, si mimi. Nijalie nikae moja kwa moja na Neno Lako. Mnaona? Ama labda ninge kuwa asiyeamini ambaye huwazia tu, ‘Vema, kama—kama . . . vema, kwa nini wengine wao wasiseme hivyo?’ Mnaona? Wala mimi si—sitaki kuwa hivyo. Nataka kuwa mwamani. Nataka kuwa hivyo. Ninaliona Neno la Mungu la wakati huu. Ninamwona Mungu ndani Yake. Basi, Bwana, nifanye sehemu ya Neno hilo. Nifanye sehemu Yake. Ninataka kuwa sehemu Yake.” Bwana awabariki.

³¹⁴ Basi hebu tuombe. Na kila mtu, wewe ji—jiombe, nami nitawaombea. Je! mlijua, siku moja tuta— . . . hatutakuwa pamoja hapa, labda, kwa muda kidogo. Wengine wetu watatwaliwa, na hatutakuwa pamoja. Kuna wengine wetu hapa, ambapo, wengine wetu wanazeeka. Wengine wetu, hatujui. Hata walio vijana hufa. Tunakufa kwenye umri wo wote. Hatuna budi kutenganishwa, na jambo hili halina budi kutatuliwa. Nawe huwezi tu kulipata jambo hili pale vivi hivi, huna budi kuja wakati ungali na akili timamu.

³¹⁵ Mnasema, “Vema, kabla tu sijafa, kama tu naweza kuliona Hilo.” La, usifanye jambo hilo. Huenda hata usiwe na akili timamu wakati huo. Huenda ukauawa kabla hujafika nyumbani, katika ajali. Huenda ukafa kwa ugonjwa mbaya wa moyo. Hatujui litakalotukia; Mungu tu ndiye anayeshikilia jambo hilo. Ninatumaini sivyo.

³¹⁶ Ninawaangalia watu huko nje, hata, wakiinua mikono yao dirishani. Mnaona? Naam, Mungu awabariki.

³¹⁷ “Ni—ninataka—ninataka kuwa sawa. Ni—ni—ni—ninataka kuwa sawa.” Na sasa hebu tulisahihishe, sasa, sasa hivi. Sasa, unaweza kulitatua kwa wakati mmoja, kutoka kwenye kilindi cha moyo wako, iwapo utasema kwa unyenyekevu, “Bwana Yesu, haidhuru ni kitu gani, ama asemacho mtu mwingine, Neno Lako litakuwa la kwanza maishani mwangu. Ninalitaka katika maisha yangu. Wewe ni Neno. Biblia ilisema jambo hilo, nami ninaamini ya kwamba Biblia ni Neno la Mungu. Nami ninajua kanuni za imani na mafundisho ya sharti, ambayo yameingizwa ndani Yake, yamelifanya lundo la unafiki. Bwana, nitakase na upuzi kama huo, na unijalie kuwa Wako kabisa.

Ninainua mikono yangu Kwako. Ninainua moyo wangu Kwako, sauti yangu Kwako, dua yangu Kwako. Mungu, nirehemu.”

³¹⁸ Nami mikono yangu iko juu, pia, Bwana. Nioshe, Ee Bwana, kutokana na kutokuamini kwote.

³¹⁹ Ingawa huenda asinipe Ngu—Nguvu ya kutembea kama Henoko na isinilazimu kufa, bali kwenda katika matembezi ya alasiri kisha niende Nyumbani pamoja Naye; lakini, Mungu, ninaamini jambo hilo litatukia, kwa sababu ninajua kunapaswa kuwe na Kunyakuliwa katika siku ya mwisho, nayo kazi itafupishwa.

³²⁰ Pia, Baba, ndivyo isemavyo kalenda yetu, miaka thelathini na sita zaidi na kazi itakwisha, nawe itakubidi kuja siku moja katika wakati huo la sivyo hakuna mwenye mwili atakayeokolewa. Halafu tunaambiwa, na wenye elimu ya miaka na wa—watu wawnaochunguza mambo kama hayo, ya kwamba tumeendelea sana kwa miaka mingi, mingi sana kutoka hapo, miaka mingi sana mbele. Wao wanatwambia, kwa kalenda, ya kwamba tumeendelea mbele zaidi ya hapo; labda ni miaka kumi na mitano ama ishirini iliyosalia. Sijui, Baba. Bali ninajua, hata kulingana na kalenda yetu, tumekaribia sana kufika kule.

³²¹ Ninaona ambapo hapawezi kuwa na tumaini lo lote lililosalia, Bwana. Kutakuja nini-hii...Kama wakianza kurushiana hayo mabomu wao kwa wao, Bwana, ha—ha—hakutakuweko na uwanja wa vita. Wao, wao wataangamizana. Naam, Bwana, zinaning’inia kule, na hata hivyo Biblia inasema mbingu zote na nchi zitateketezwa. Mungu, ninaona saa hiyo ikikaribia.

³²² Ninafikiri juu ya mauaji ya Rais, halafu namwona mtu huyo mwingine mwovu akiingia, bila ya kumwacha mtu huyo apate kushtakiwa, nao wakampiga risasi, katika mauaji ya kinyama. Ee Mungu, mmoja ana hatia kama yule mwingine. Wao hawana haki ya kufanya jambo hilo. Uovu katika taifa letu wenyewe, linadhaniwa kuwa ni taifa la Kikristo, sisi ni mfano mbaya namna gani, Bwana, la Mkristo. Tusamehe, Bwana, dhambi zetu.

³²³ Tusaidie, Ee Mungu, hasa Kanisa Lako, hao ambao wamebatizwa kuwa Mwili huo wa kisiri wa Kristo. Ambao, “Roho ndiye anayehuisia,” Wewe ulisema. Basi kama vile Mwana wa Adamu alivyopaa, vivyo hivyo Mwili Wake utapaa. Naye ndiye Kichwa; Kanisa Lake ndio Mwili.” Ee Mungu, kichwa ndicho kinachouongoza Mwili. Basi na Kichwa cha Neno kiuongoze Mwili wa Kristo. Nami naomba niwe sehemu ya Mwili huo, Bwana.

³²⁴ Ninawaombea hawa walioiinua mikono yao, na hao wote waliopo hapa na wote watakaokuwa kwenye kanda. Bwana Mungu, ninaomba kwa uaminifu. Waingize, Bwana. Iangalie mioyo yao. Unajua kile walicho. Lakini, kama mtumishi

Wako, ni—ninawaombea hawa watu, Bwana. Ni—ninawapenda. Ninawapenda.

³²⁵ Nami ni—ni—ninajaribu tu kufanya jambo hili kwa maana nilijihisi agizo Lako ni kwamba nilifanye. Kwa hiyo, Baba, mimi hapa, nikifanya vizuri niwezavyo... Nisamehe makosa yangu dhaifu, Bwana. Naomba ya kwamba Wewe—Wewe utanipa nguvu, ili kwamba nipate kulifanya dhahiri zaidi kwa watu.

³²⁶ Basi kaa pamoja nasi hapa kwenye Maskani, usiku wa leo. Waangalie watu hawa, Bwana, hao walioinua mikono yao Maskanini. Nichunguze, Ee Bwana, na unijaribu. Na kama kukiwa na lo lote baya ndani yangu, nioshe, Baba. Tujalie. Takasa kanisa hili.

³²⁷ Tutakase sote, Bwana, ili kwamba Neno lifanyike mwili miongoni mwetu na lijulikane kwa walimwengu katika siku hii. Tujalie, Baba. Kwa kuwa, ninaweka hili, pamoja na nafsi yangu, na fungu hili la maneno, na pamoja na kusanyiko hili, pamoja na Neno Lako na ahadi Yako, kwa ajili ya wokovu wa nafsi zetu, katika Jina la Yesu Kristo. Tujalie, Bwana.

³²⁸ Jalia kwamba Nguvu za Mungu zije juu yetu na kututia mafuta, moja kwa moja kutoka mchungaji hadi kwa bawabu, na kila mtu aliyeko. Jalia Roho Mtakatifu aje na kuchukua mahali Pake mioyoni mwetu, na kuchukua kila ahadi ya Mungu na kutufunulia ya kwamba Neno Lako ni Kweli. Katika Jina la Yesu naomba.

³²⁹ Basi wakati tumeinamisha vichwa vyetu. “Ninaweza...” Nataka tu mpiga kinanda, kama akiweza, kutupa sauti ya wimbo huu, “Ninaweza kumsikia Mwokozi wangu akiita. Aniongozako nitafuata.” *Aniongozako Nitafuata.*

...Mwokozi wangu akiita, (Yeye ni nini? Neno!)

Ninaweza kumsikia Mwokozi wangu akiita,
Ninaweza kumsikia Mwokozi wangu akiita,
(sasa yakane mafundisho yako ya sharti na kadhalika)

Uchukue msalaba wako na ufu-...

³³⁰ “Yeye asiyeuchukua msalaba wake na kunifuata Mimi, Neno, hastahili kuwa mwanafunzi Wangu.”

Aniongozako (kurudi kwenye Biblia, ambako atakuongoza)...-tafuata,

Aniongozako nitafuata,

Aniongozako nitafuata,

Nita...(kama ni kwenye kidimbwi, katika Jina Lake; kama ni madhabahuni, kuondoa aibu yangu!)...kote.

³³¹ [Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Aniongozako Nitafuata*—Mh.]

... Yeye kupitia hukumu, (hiyo ni sasa hivi)
Nita-...

³³² Wewe uko upande gani? Unaona kitu gani unapojiangalia katika Biblia inayokuonyesha ulivyo wewe, kioo cha Mungu cha kujiangalia, kama mimi ninahukumiwa sasa na Neno?

Nitaambatana...

³³³ “Nitaambatana na Neno, haidhuru litanigharimu nini. Ninapitia katika hukumu za Mungu. Kama itanibidi kuchukua moja ya nafasi hizo, nifanye mwamini, moja kwa moja, kwenye Neno.”

... pamoja Naye, pamoja Naye kote.
Kwa maana aniongozako ni-...

³³⁴ Sasa wazia jambo hilo, kwa makini sana sasa.
“Aniongozako...”



AINA TATU ZA WAAMINI SWA63-1124E

(Three Kinds Of Believers)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, tarehe 24 Novemba, 1963, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Hii tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 2004 na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1994 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org